SportPesa
TZS. 537,737,060
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



## DC amsimamisha kazi mwenyekiti wa kijiji tuhuma kuchochea fujo

UKURASA 3


Uviko-19, Wamachinga wasitugombanishe
Ukurasa 14
BUFE
IJUMAA OKTOBA 1, 2021
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
KILELE SIKU YA WAZEE DUNIANI
Tanzania imeshafikia mengi ya kujivunia?
Ukurasa 12
TARI yafungua kituo Dodoma kuweka sawa uzalishaji shambani Kanda Kati
• Waziri Mkenda: Jiandaeni kwa mapya
• Mkurugenzi: Tumejipanga, tunakuja
Na Elizabeth Zaya, aliyekuwa Dodoma
TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), miongoni mwa shughuli zake inazozifanya ni utafiti kwa ajili ya kuendeleza, kuinua na kutoa mchango katika kuboresha sekta ya kilimo nchini, ili ilete tija.
Hivi karibuni asasi hiyo imezindua kituo mahiri cha usambazaji wa teknolojia za kilimo kilichopo Nzuguni, jijini Dodoma, kwa ajili ya Kanda ya Kati, kitakachotumika kushughulikia mahitaji ya wakulima, ikiwamo elimu kwa vitendo kwa wakulima katika eneo hilo wakati wote.
Lengo kubwa la kuwapo kituo hicho ni kuhakikisha kinatoa mchango katika kuboresha sekta ya kilimo nchini, kwa kuongeza, hivyo kutimiza agizo la Wizara ya Kilimo la kuongezwa tija na uzalishaji katika sekta kilimo.
kwa usahihi, sambamba na viuatilifu.
Profesa Mkenda anayajumuisha yote, ni zao la kukosekana elimu bora ya huduma za kutumia ugani. Ana ufafanuzi: "Kwa hiyo, naamini kwamba kuanzishwa kwa kituo hiki kutaongeza ushirikiano kati ya wakulima, wagani na wadau wengine na kimeanzishwa muda mwafaka wakati wizara imeweka mkakati wa kuimarisha huduma za ugani nchini."
"Ni rai yangu kwa viongozi wa mikoa iliyo katika Kanda ya Kati watumie kituo hiki kuwajengea uwezo kwa vitendo maofisa ugani ili wasaidie kuwajengea uwezo wakulima katika maeneo yao ya kazi kusaidia kuongeza uzalishaji na tija, kuchangia kuwa na uhakika wa chakula, kipato, lishe bora na ukuaji wa uchumi kwa mtu mmoja mmoja, kaya na taifa kwa ujumla," anafafanua.
Profesa Mkenda anaeleza imani yake kwamba, kituo hicho cha kusambaza teknolojia za kilimo, kitaendeleza malengo yake mahsusi ya mafunzo kutumia teknolojia za kilimo bora, mbegu za kisasa, kupanda kwa nafasi na matumizi sahihi ya mbolea na viuatilifu.

UKURASA 11

Ijumaa Oktoba 1, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580719

www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Mbivu, mbichi kesi ya Sabaya



**Hukumu** madai ya unyang'aji leo, shahidi kesi uhujumu adai kumwona akiingia gereji... *Endelea ukurasa 2 na 4*

# Samia ataka maelewano, ukaribu serikali na NGO



UKURASA 2




Rais Samia Suluhu Hassan, akiongoza Watanzania kuaga mwili wa aliyekuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji, marehemu William Tate Ole Nasha, katika viwanja vya Bunge, jijini Dodoma jana. Habari Uk. 4. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

UKURASA WA 4

## MADEREVA WA TANZANIA WADAI KUPIGWA MALAWI

MADEREVA wa malori ya mizigo wa Tanzania wanadai kutekwa, kupigwa, vioo vya magari yao kuvunjwa kwa chupa za bia na kuzuiliwa kusafiri ...

UKURASA WA 5

## SERIKALI YAONYA BAA NA KUMBI KELELE ZA MUZIKI

SERIKALI imezionya baa na kumbi za starehe, ambazo zimekuwa zikikiuka sheria kwa kushindwa kudhibiti kelele, kwenye shughuli zao kwa kuwa madhara ya kiafya kwa jamii ni makubwa...



UKURASA WA 4

## MAJALIWA ABAINISHA CHANZO KIFO CHA NASHA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema chanzo cha kifo cha aliyekuwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), William...

UKURASA WA 7

## DAWASA KUSAJILI MAGARI HUDUMA BINAFSI MAJI TAKA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) imetangaza kufanya usajili kwa watoa huduma binafsi wa magari na kutoa vibali vya uendeshaji kuanzia...



## Mchengerwa awakalia kooni wakuu utumishi

UKURASA 3

**MICHEZO** SIMBA, DODOMA JIJI MAJARIBUNI UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6




Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Utawala wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB), Diana Myonga, akipata chanjo ya Covid-19, wakati wa uchanjaji uliofanywa na benki hiyo kwa kushirikiana na Hospitali ya Kairuki Mikocheni, katika makao makuu ya TCB Makumbusho, mkoani Dar es Salaam jana, kwa ajili ya wafanyakazi wake, ndugu, jamaa na marafiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia ataka maelewano serikali, NGO

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema kumekuwa na hali ya kutoelewana na kuaminiana kati ya serikali na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGO).

Hata hivyo, amesema kupitia mkutano mkuu wa mwaka wa jukwaa la mashirika hayo ambao aliuhudhuria, hali hiyo itaondoka.

Akizungumza jana jijini hapa kwenye mkutano huo, Rais Samia alisema kuwa serikali imejipanga kuhakikisha inaendelea kuboresha mazingira ili kustawisha utendaji kazi na ufanisi wa mashirika hayo.

"Mara kadhaa kumekuwa na hali ya kutoelewana na kuaminiana kati ya serikali na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, kupitia mikutano hii, hali hiyo itaondoka. Tunaamini kwenye majadiliano hakuna linaloharibika," alisema.

Aidha, Rais alitaja mambo manne muhimu kwa NGO, ikiwamo kuongeza uwazi na uwajibikaji na kufanya kazi kulingana na vipaumbele na mipango ya serikali.

Akizungumzia mambo hayo, alisema mashirika hayo yanapaswa kuoanisha mipango yao na vipaumbele na mipango ya kitaifa ya serikali.

"Yaani mashirika yasiyo ya kiserikali yafanye kazi kwa kuangalia mipango ya kitaifa na Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano wa Maendeleo, naomba msome mpango huu muutafsiri katika kazi zenu ili kuutekeleza kwa pamoja serikali na ninyi na kwa haraka," alisema. Alihimiza mashirika hayo kuongeza uwazi na uwajibikaji kwenye utendaji kazi.

"Mwanzoni nimeeleza kwamba mashirika yaliyopata usajili ni zaidi ya 11,000 na yanayofanya kazi ni 4,663 tu, utakuta kuna mashirika takribani 7,000 aidha hayajulikani yanafanya nini au yamekufa au vinginevyo."

"Hii ni kwa sababu mashirika mengi yanaanzishwa kwa ajenda iliyopo duniani kwa wakati ule, ulimwengu ukieleka kwenye mazingira yaanzishwa mashirika mengi ya mazingira, ulimwengu ukizungumza watoto na haki zao mashirika mengi yatasajiliwa ya mrengo huo na hii kwa sababu wanajua kuna fedha ipo mahali."

"Nikianzisha taasisi hii fedha zitakuja, sasa mashirika ya aina hiyo ambayo hayajulikani yanafanya nini, hivyo mnatakiwa kwenda na ajenda za ulimwengu kama malengo 17 ya Maendeleo Endelevu, lakini tuende na mipango ya serikali, tukienda hivyo wanaotoa fedha watawaelewa vizuri," alisema.

Kadhalika, aliagiza mashirika hayo hususani ya ndani kupunguza utegemezi.

Aliitaka wizara kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCONGO) kutengeneza mipango mkakati ambao taasisi hizo zitatafuta fedha zao na kujitegemea. "Wito wangu wa nne mashirika fanyeni kazi zinazoendana na tamaduni, mila na desturi na maadili ya kitanzania, pia endeleeni kuzingatia sheria zinazosimamia shughuli za mashirika," alisema.

Alisema mashirika hayo yana mchango mkubwa kwa maendeleo na ustawi wa taifa ambapo kati ya mashirika yaliyosajiliwa 11, 603, yanayofanya kazi ni 4,663 na yametoa ajira za moja kwa moja 17,836.

"Hii ndiyo faida ya kwanza ya mashirika haya kama serikali isingeruhusu kuwapo kwa mashirika haya ajira hizi zisingekuwapo na ungekuwa mzigo wa serikali, pia ni kichocheo cha maendeleo ya kiuchumi na kuongeza kasi ya utoaji huduma mbalimbali za kijamii," alisema. Alisema mwaka jana ulifanyika uchambuzi wa mapato na matumizi kwa mashirika 803 ambayo ilibainika mapato yalikuwa Sh.trilioni 1.2 na matumizi yalikuwa Sh. trilioni moja na hiyo inadhihirisha umuhimu wake.

Kuhusu misamaha ya kodi, alisema kuna baadhi ya taasisi zinastahili kupata misamaha ya kodi hivyo serikali imeanza kulifanyia kazi.

"Kwa mashirika yanayofanya kazi kwa hisani tunamalizia kuandaa kitini kinachotoa mwongozo wa namna yatanufaika na misamaha ya kodi," alisema.

Alikubaliana na ombi la mashirika hayo kushirikishwa kwenye mapambano ya UVIKO-19 na kuwataka kulibeba pia suala la sensa ili kuhamasisha wananchi kuhesabiwa.

Awali, akizungumzia mchango wa mashirika hayo, Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Dk. John Jingu, alitaja kikwazo kikubwa kwa mashirika hayo ni utegemezi wa misaada kutoka nje ya nchi.

Mwenyekiti wa NaCONGO, Dk. Lilian Badi, alisema sekta ya mashirika hayo inakabiliwa na vikwazo mbalimbali ambavyo vinakwamisha ufanisi wa utekelezaji wa shughuli za mashirika hayo nchini.

"Changamoto hizi ni pamoja na ya kupatikana misamaha ya kodi, kwa mashirika yasiyo ya kiserikali, kuna changamoto ya muda unaotumika kupata vibali kwa ajili ya kutekeleza miradi na afua mbalimbali katika sekretarieti za mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa," alisema.

# Mbivu mbichi hukumu kesi ya Sabaya

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, leo inatarajia kutoa hukumu katika kesi ya jinai namba 105 ya unyang'anyi wa kutumia silaha inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya (34).

Washtakiwa wengine katika shauri hilo ni Silvester Nyegu(26) na Daniel Mbura(38), ambao wanakabiliwa na mashtaka matatu ya unyang'anyi kwa kutumia silaha.

Kesi hiyo ilinguruma kwa siku 35 mfululizo mbele ya Hakimu Mwandamizi wa mahakama hiyo, Odira Amworo hadi kufikia tamati.

Upande wa Jamhuri ulikuwa na mashahidi 11 na vielelezo 10 vya ushahidi na viliwasilishwa mahakamani kama sehemu ya ushahidi.

Mashahidi wa upande wa utetezi, walikuwa watatu na walijitetea kwa njia ya kula kiapo na kuwasilisha baadhi ya nyaraka kama vilelezo vya ushahidi.

Upande wa Jamhuri, uliwakilishwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Tumaini Kweka, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Abdalah Chavula, Wakili wa Serikali, Baraka Mgaya, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Filex Kwetukia na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Tersila Gervas.

Kwa upande wa mawikili wa utetezi, waliwakilishwa na Mosses Mahuna, Duncan Oola, Silvester Kahunduka, Fredolin Gwemelo, Edmund Ngemela na Jeston Justine.

Ole Sabaya na wenzake wawili, wanakabiliwa na shtaka la kwanza la unyang'anyi wa kutumia silaha. Ilidaiwa mahakamani hapo kuwa Februari 9, mwaka huu, katika Mtaa wa Bondeni jijini Arusha, washtakiwa hao waliiba fedha kiasi cha Sh. 2,7690,000 mali ya Mohamed Saad na baada ya kufanya wizi huo walitumia silaha ya bunduki kuwatisha watu waliokuwa kwenye duka hilo.

Shtaka la pili, ni la unyang'anyi wa kutumia silaha, ilidaiwa kwamba washtakiwa hao kwa pamoja wakiwa Mtaa wa Bondeni jijini Arusha, waliiba fedha kiasi cha Sh. 390,000 mali ya Bakari Msangi na baada ya wizi huo walimfunga na pingu, wakampiga makofi, mateke, ngumi na wakatumia silaha ya bunduki kumtisha ili wabaki na fedha walizochukua kutoka kwake.

Shtaka la tatu ni la wizi wa kutumia silaha. Ilidaiwa mahakamani washtakiwa hao kwa pamoja Februari 9, mwaka huu, wakiwa katika Mtaa wa Bondeni jijini Arusha, waliiba simu moja aina Tekno Pop 1, na fedha kiasi cha Sh.35,000 mali ya Ramadhani Rashid na baada ya kufanya uhalifu huo, walimpiga makofi, ngumi, mateke na walitumia silaha kumtisha ili wapatiwe fedha na mali walizoiba.

## HABARI KITAIFA

# Mchengerwa awakalia kooni wakuu utumishi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mohamed Mchengerwa, ameagiza watendaji wa wakala za serikali kuwashusha vyeo au kuwaondoa maofisa utumishi watakaobainika kutopeleka taarifa za kupandishwa madaraja watumishi.

Aidha, amewataka kuondoa urasimu katika utoaji wa huduma ambao unachangia uwapo wa vitendo vya rushwa kwenye maeneo yao.

Mchengerwa aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akifungua kikao kazi cha watendaji wakuu wa wakala hizo. Aliwataka watendaji hao kufuatilia katika maeneo yao kama kuna ofisa ambaye hajapeleka taarifa za kupandisha madaraja watumishi walio chini yao washushwe vyeo mara moja.

“Kama kuna ofisa utumishi ambaye hakuleta taarifa za kupandisha madaraja watumishi walio chini yake ashushwe cheo mara moja au aondolewe apelekwe mtu mwingine,” alisema.

Mchengerwa alisema serikali inajitahidi kulinda maslahi ya watumishi na ilishatoa maelekezo ya kupunguza malalamiko ya watumishi kwa kuwalipa stahiki zao na waliokidhi vigezo vya kupandishwa madaraja.

“Nitashangaa kuona baadhi ya taasisi watumishi wake wana malalamiko kwa sababu tulishatoa maelekezo watu walipwe na tumeona dhamira ya Rais wetu Samia Suluhu Hassan katika kipindi kifupi tu amepandisha madaraja watumishi 180,000 kwa mara moja hii haijawahi kutokea,” alisema.

“Awamu hii hatutegemei kusikia eti ni maelekezo kutoka juu. Kama kweli umepewa maelekezo basi yawe kwenye maandishi ili uwe salama. Unakuta hadi kwenye utekelezaji wa miradi unaambiwa ni maelekezo kutoka juu.

Sasa kasimamieni miradi ikamilike kwa wakati na kwa ubora unaotarajiwa. Tunataka tuone Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere unazinduliwa 2022,” aliongeza.

Sambamba na hayo, aliagiza maofisa ununuzi kutokaa sehemu moja kwa muda mrefu bali wazunguke na kuona wengine wanavyofanya kazi na hiyo itasaidia kuongeza uwajibikaji na uelewa.

Kuhusu watumishi hewa, Mchengerwa aliwataka watendaji hao kutotumia mwanya wa kuajiri vibarua au watumishi wa mkataba kama njia ya kuweka mwanya wa watumishi hewa.

“Katika bajeti ya 2021/22, serikali iliomba kibali cha kuajiri watumishi 46,000 na mpaka sasa waliojiriwa hawazidi 10,000, hivyo kama mna uhitaji wa wafanyakazi ombeni kibali cha kuajiri na si kutumia vibarua au watumishi wa mkataba ili kuweka mwanya wa watumishi hewa,” alisema.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Prof. Sifuni Mchome, alisema lengo la kikao hicho ni kujadili masuala ya wakala, mafanikio na kero ili kuzitafutia ufumbuzi.

## DC amsimamisha kazi mwenyekiti kwa tuhuma za kuchochea vurugu

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Monduli mkoani Arusha, Frank Mwaisumbe, amemsimamisha kazi Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Eng'aroji, Kata ya Lepurko, Ngarama Mapema, kwa tuhuma za kuhamasisha wananchi kuushambulia kwa mawe msafara wake.

Jana, Mwaisumbe alisema Septemba 24, mwaka huu, akiwa na kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya hiyo wakienda katika kijiji hicho, ghafla alianza kushambuliwa kwa mawe.

“Nikiwa nahutubia wananchi hao, walitaka ufafanuzi kuhusu mgogoro wa ardhi kati yao na mkazi mwenzako Paul (mfanyabiashara wa madini) wanayemtuhumu kujimilikisha ardhi yao yenye ukubwa wa ekari 700.

“Niliwajibu kuwa siwezi kuongelea jambo lililopo mahakamani, ndipo walipopandwa na jazba wakidhani namtetea na kuanza kunishambulia kwa mawe,” alisema.

Inaelezwa kuwa wananchi hao pia walifanya uharibifu wa kukatakata mabomba ya maji na kutoboa matangi katika eneo la mfanyabiashara huyo wa madini.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya, katika tukio hilo, hakuna mtu aliyejeruhiwa ila baadaye ofisi yake ilifanya uchunguzi na kubaini kwamba Mwenyekiti huyo alishiriki kuandaa na kuwachochea wananchi kuwazomea viongozi wanaofika kijijini hapo kwa maslahi yao.

Alisema mbali na yeye (DC) kupopolewa kwa mawe, pia Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, na Mkuu wa Wilaya aliyepita, waliwahi kukumbwa na kadhia ya kuzomewa kijijini hapo.

Kutokana na tukio hilo pamoja na malalamiko ya baadhi ya wananchi, Mwaisumbe ameiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Mkuu wa Polisi wa Wilaya hiyo (OCD), kuchunguza tuhuma zinazomkabili mwenyekiti huyo na kuchukua hatua.

Akizungumza kwa njia ya simu, Mwenyekiti huyo, Ngarama, alisema hatambui taarifa za kusimamishwa uongozi wake na Mkuu wa Wilaya yeye bado ni kiongozi wa wananchi na anaendelea na majukumu yake kama kawaida.

Siku chache zilizopita, baadhi ya wananchi wa kijiji hicho cha Eng'aroji, waliandamana hadi kwa Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Arusha, Musa Matoroka, wakikitaka chama hicho kuingilia kati mgogoro huo.

Alipoulizwa kuhusu taarifa za wananchi hao kukimbilia CCM kutafuta msaada, Matoroka alisema: “Ni kweli wamekuja na nimewasikiliza na malalamiko yao yatafikishwa ngazi husika, kwa ajili ya kuyafanyiwa kazi.”


## ATNOTISI/ TANGAZO

**MUDU COMPANY LTD, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD, ,LEGENDS AUCTION MART LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,CHAMPION AUCTION MART,MAKI RECOVERIES LTD,PSALM AUCTION MART,MALAPA AUCTION MART,HEDANE ENTERPRISES LTD,KILICRAALS AUCTIONEER, DESTENI COMPANY LIMITED, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS,JY AUCTIONEERS CO.LTD, SMARKCORE GROUP LTD, WAUNGWANA AUCTION MART LTD, BEST GROUP LTD, NGOMENI AUCTION MART,MOPEH COMPANY LTD,KOTI BROTHERS LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya benki ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| ASNA SAIDI MJEMA | NYUMBA | ASNA SAIDI MJEMA | VIGWAZA-CHALINZE | 15/10/2021 NA KUENDELEA |
| KHALID RAI MWARAI | GARI T771 CQL | KHALID RAI MWARAI | TABATA | 15/10/2021 NA KUENDELEA |
| REAL TASTE BAKERY | NYUMBA | THEODORY THEONEST BYABATO | KIBAMBA-UBUNGO | 15/10/2021 NA KUENDELEA |
| BERNAD MONGI TARIMO | NYUMBA | BERNAD MONGI TARIMO | KAGERA-MAGOMENI | 18/10/2021 NA KUENDELEA |
| RAJABU SHABAN RAJABU | NYUMBA | RAJABU SHABAN RAJABU | MBWENI | 15/10/2021 NA KUENDELEA |
| TANDI SAM SIKALANGWE | PAGALE-NYUMBA | TANDI SAM SIKALANGWE | PUGU BOMBANI | 16/10/2021 NA KUENDELEA |
| RAJABU MOHAMEDI MUOMBWA | NYUMBA | RAJABU MOHAMEDI MUOMBWA | MSONGOLA YANGE YANGE | 15/10/2021 NA KUENDELEA |
| EVA JOHN MIHAYO | NYUMBA | DIDAS DONATUS NYAKIMWE | PUGU KINYAMWEZI | 15/10/2021 NA KUENDELEA |
| VALENCE WILLIAM GALINOMA | NYUMBA | VALENCE WILLIAM GALINOMA | MOSHONO | 15/10/2021 NA KUENDELEA |
| PRECIOUSEMMY VICTOR SHITINDI | GARI T130 DQJ | PRECIOUSEMMY VICTOR FRANCIS | ARUSHA | 15/10/2021 NA KUENDELEA |
| HAMAD ABDALLAH MNEMBWE | NYUMBA | HAMAD ABDALLAH MNEMBWE | TANDALE | 15/10/2021 NA KUENDELEA |
| BERNARD KEMBO NDIEGE | NYUMBA | BERNARD KEMBO NDIEGE NA ASHURA SAID MCHOPA | KIGAMBONI | 16/10/2021 |
| MUSTAPHA ABDALLAH ATHUMAN | NYUMBA | MUSTAPHA ABDALLAH ATHUMAN | MSONGOLA | 15/10/2021 NA KUENDELEA |
| OMARY YUSUPH HEMED | NYUMBA | OMARY YUSUPH HEMED | SALA SALA | 18/10/2021 NA KUENDELEA |
| FREDRICK BALTAZARY PETER | NYUMBA | FREDRICK BALTAZARY PETER | ULONGONI | 19/10/2021 NA KUENDELEA |
| BENJAMIN PETER MUSHI | NYUMBA | BENJAMIN PETER MUSHI | KIVULE-ILALA | 19/10/2021 NA KUENDELEA |
| IBRAHIM MPANDA MPANDA | NYUMBA | HAMIS MPANDA | MBEZI MAKABE | 20/10/2021 N A KUENDELEA |

### MASHARTI YA MNADA

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwamnunuziatashindwakutimizashartilolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwapesayoyotealiyokwishailipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.0768672367/0713604044/0784252048/0713836150/0785242219
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.

216486102

# Majaliwa abainisha chanzo kifo cha Ole Nasha

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema chanzo cha kifo cha aliyekuwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), William Ole Nasha, ni shinikizo la damu.

Ole Nasha alifariki dunia mapema wiki hii nyumbani kwake, Medeli jijini Dodoma na aliagwa jana huku Rais Samia Suluhu Hassan akiongoza mamia ya waombolezaji katika viwanja vya Bunge jijini hapa.

Akitoa salamu za rambirambi kwa niaba ya ofisi yakemara baada ya ibada ya kuaga mwili, Majaliwa alisema serikali imepoteza mtu mchapakazi.

"Taarifa za msiba huu zimekuja katika hali ya kushtua sana na hata maumivu yake yamekuwa makali sana. Kwa maana hiyo niwaombe wanafamilia kuwa wavumilivu katika kipindi hiki kigumu," alisema Majaliwa.

Majaliwa alisema alisema hadi umauti unamkuta, hakuna aliyekuwa anategemea kuwa kifo chake kingekuja kwa namna ya kushtua kiasi hicho.

"Siku ya kifo chake hata dereva wake anasema alimshusha nyumbani kwake akiwa mzima na yeye kuendelea na mambo yake. Hata majirani zake wanadai alitoka kwenda kula na kurudi salama lakini aliporudi nyumbani baada ya kutoka kula wakati akipandisha ngazi akiwa ghorofa ya pili, aliishiwa nguvu na kuanguka.

"Wakati majirani wanatafuta namna ya kumsaidia ndipo umauti ukamkuta. Waziri wa Afya (Dk. Dorothy Gwajima) alituma gari na wataalamu wa afya lakini walimbeba akiwa tayari ameshapoteza maisha," alisema Majaliwa.

Alisema ripoti ya madaktari iliyotolewa imeonyesha kuwa kifo chake kimesababishiwa na shinikizo la damu.

"Mheshimiwa Rais, kwanza nikupe pole sana wewe kwa kumpoteza mtu ambaye alikuwa akitekeleza ipasavyo majukumu uliyomkabidhi katika sekta ya uwekezaji," alisema Majaliwa.

Alisema Ole Nasha kupitia taaluma yake ya sheria, aliisaidia sekta ya uwekezaji katika kutatua kero mbalimbali pamoja na migogoro iliyokuwapo baina na wizara na wawekezaji.

"Hata siku hii alipokutwa na umauti alikuwa anatoka Bagamoyo kutekeleza sehemu ya majukumu yake katika masuala ya uwekezaji," alisema.

Makamu wa Rais, Dk. Philp Mpango, alisema Ole Nasha atamkumbuka kama mtu ambaye alikuwa tayari muda wote kufanya kazi na wenzake.

"Nakumbuka mimi nilionana naye mara ya mwisho Septemba 22, mwaka huu, kule Kigoma ambako Mweshimiwa Rais uliponituma kwenda kufungua maonyesho ya SIDO na tuliagana naye vizuri. Alikuwa anapenda kunitania kwa kuniita shemeji," alisema.

Pia alisema wakati (Dk. Mpango) akiwa Waziri wa Fedha na Mipango, alikuwa anamsaidia kutetea miswada mbalimbali ya wizara yake bungeni.

Akitoa salamu kwa niaba ya Manaibu Waziri wote, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisema Ole Nasha alikuwa mtu aliyekuwa tayari kufanya kazi yoyote na wakati wote.

"Nakumbuka wakati wa uhai wake wakati ambao tulikuwa tukikosa mtu wa kwenda kujibu maswali bungeni yeye ndiye alikuwa anaifanya kazi hiyo tena kwa ufanisi. Sisi mawaziri tumepoteza mtu muhimu," alisema Ulega.

Spika wa Bunge Job Ndugai, alisema Bunge limempoteza mwanasheria na mbunge makini aliyekuwa tayari wakati wote kuitumikia nchi yake.

"Mimi nimemfahamu Ole Nasha kabla hata hajawa Mbunge akiwa anafanya mambo yake ya sheria katika maeneo mbalimbali kipindi kile ambacho palikuwa na mgogoro mkubwa sana baina ya wafugaji na wakulima kule Morogoro, wakati huo nikiwa Mwenyekiti wa Kamati ya bunge," alisema.

Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, alisema chama kimempoteza mtu ambaye alikuwa daraja la kutatua kero baina ya wananchi na serikali katika Jimbo la Ngorongoro.

Akitoa salamu kwa niaba ya familia, Edward Porokwa, alisema wanaishukuru serikali kwa ushirikiano waliowapatia toka msiba huo wa kuondokewa na mpedwa wao huyo ulipotokea.

## Madereva wa Tanzania wadai kupigwa Malawi

**Na Thobias Mwanakatwe**

MADEREVA wa malori ya mizigo wa Tanzania wanadai kutekwa, kupigwa, vioo vya magari yao kuvunjwa kwa chupa za bia na kuzuiliwa kusafiri kurejea nchini, kufuatia mgomo wa madereva wa Malawi unaoendelea.

Video iliyosambaa kwenye mitandao ya kijamii kuanzia jana, imeonyesha baadhi ya magari yenye namba za Tanzania yaliyoegeshwa eneo la Kanengo Lilongwe nchini Malawi yakiwa yamevunjwa vioo.

Miongoni mwa magari yaliyoonekana katika video hiyo yalikuwa yamevunjwa kioo ni la kampuni ya Global Leader Enterprises (T) Ltd namba T 177 DKR ambalo kioo cha mbele na cha upande wa dereva kimevunjwa.

Mmoja wa madereva wa Tanzania ambaye hajajitambulisha jina lake, amesikika katika video hiyo kuwa kutokana na vurugu Malawi wamewekwa kwenye mayadi ya watu ambako hawakujui bila msaada wowote.

Alisema madereva wa Malawi wamegoma wakishinikiza nyongeza ya mishahara na wameteka magari ya nchi mbalimbali yasisafiri kutoka nchini humo wakitaka hadi serikali yao iwasikilize kilio chao.

"Gari zimevunjwa vioo kwa chupa za bia, sababu ni mgomo wa madereva wa Malawi ambao wanadai nyongeza ya mishahara, madereva wa Tanzania wengine wamepigwa nondo za mikono na wengine wamevunjiwa vioo vyao vya magari," imesikika sauti ya dereva mmoja akilalamika katika video hiyo.

Madereva hao wa Tanzania wameiomba serikali iwasaidie kutokana na hali ngumu ya maisha wanayokabiliwa nayo kutokana na vurugu hizo kwani madereva wa Malawi hawataki kuwaelewa na serikali yao. Balozi wa Tanzania nchini Malawi, Benedicto Mashimba, juzi alikutana na madereva wa Tanzania eneo la Kanengo-Lilongwe kuzungumza nao kuhusu kadhia hiyo.

Kwa mujibu wa Balozi Mashimba, vurugu nchini Malawi zilianza Jumatatu na kwamba hata hivyo madereva wapo salama na kwamba hakuna taarifa ya majeruhi yeyote.

Aidha, polisi nchini Malawi wametoa idhini watu waendelee na safari zao, Balozi Mashimba akifuatilia hatua zinazochukuliwa na serikali ya Malawi kuhakikisha usalama wa Watanzania kupitia Wizara yao ya Mambo ya Nje.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki wa Tanzania, Emmanuel Buhohela, alipoulizwa kuhusiana na tukio hilo alisema serikali inalifuatilia.



Baadhi ya madaktari ambao ni wanachama wa Chama cha Madaktari Tanzania (MAT), wakishirikiana na wadau mbalimbali kutoa huduma za afya bure kwa wakazi wa mji wa Geita. Mpango huo maalumu wa siku tatu umefadhiliwa na Kampuni ya GGML chini ya uratibu wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Geita na chama hicho. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Adai alimwona Sabaya akiingia gereji

**Na Allan Isack**, ARUSHA

MLINZI katika gereji ya mfanyabiashara Francis Mroso, Adanbest Marandu (61), amedai kwamba alimshuhudia aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, akiingia katika gereji ya mfanyabiashara huyo, Mbauda jijini Arusha, akiwa ameambatana na watu wengine sita.

Marandu, ambaye ni shahidi wa tatu wa Jamhuri, alitoa madai hayo jana wakati akitoa ushahidi wake, mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, Patricia Kisinda.

Pia shahidi huyo alidai kwamba mbali na watu hao kuingia katika eneo hilo, walitumia magari matatu likiwamo moja la serikali.

Washtakiwa wengine katika shauri hilo la uhujumu ni Sylvester Nyengu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), John Odemba, Jackson Macha(29) na Nathan Msuya(31).

Akiongozwa na Wakili wa Serikali, Tersila Gervas, alidai kwamba Januari 22, mwaka huu, majira ya saa 8:35 katika eneo hili, yaliingia magari matatu kwa pamoja yakiwa zimefuatana.

Alidai magari hayo yalikuwa na usajili wa namba T144 CZU, STL 5434 na T846 CTU na baada ya muda walishuka watu saba wakaenda ndani ya ofisi ya Mroso.

"Kilichoendelea huko ndani sifahamu kwa kuwa tangu kutoka getini hadi ofisini kwa Mroso kuna umbali wa mita 60," alidai shahidi huyo ambaye amefanya kazi katika gereji hiyo kwa miaka sita.

Pia alidai kuwa alimwona Sabaya aliingia ndani ofisi ya Mroso akizungumza na Mhasibu huku watu wengine wakiwa nje.

Alidai kwamba alimfahamu na kumtambua Sabaya kwa kuwa alikuwa akimwona kwenye televisheni kwa kuwa alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai na siku hiyo alikuwa amenyoa panki na amevaa kaunda suti ya mikono mifupi.

Januari 23, mwaka huu, alidai kuwa bosi wake alimwita na kumuuliza kwamba kama aliandika namba za magari hayo yaliyoingia katika gereji na alimwambia aliyaorodhesha katika kitabu.

Pia alidai kwamba baada ya muda Sabaya alitoka ndani akiwa ameambatana na Mroso na walitoka hadi nje ya lango la geti.

Baada ya kutoa ushahidi, Marandu alionyeshwa daftari lililotumika kuandika namba na magari ambayo Sabaya aliyoingia nayo katika gereji hiyo na kuomba mahakama kuchukua kitabu hicho kama kielelezo cha ushahidi mahakamani.

Wakili wa Utetezi, Moses Mahuna, alipinga vikali kupokewa kwa kitabu hicho kwa madai kwa madai kuwa Wakili Tersila, alitoa kitabu hicho katika mkoba wake.

Akijibu hoja hiyo, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Ofmed Mtenga, alidai wakati akitoa ushahidi wake wa msingi, shahidi aliieleza mahakama kwamba kitabu hicho alikuwa akikitumia kuhifadhi kumbukumbu na kukitunza, hivyo kisheria ni halali kupokewa kama kielelezo kwa kuwa kimepita mikononi mwake.

Baada ya kusikiliza mabishano ya kisheria, Hakimu Kisinda aliahirisha kesi hiyo kwa muda kwenda kupitia hoja za kisheria za pande zote mbili.

Akitoa uamuzi mdogo kuhusu hoja za pande hizo, Kisinda alitupilia mbali pingamizi la utetezi kwa kusema shahidi alikuwa na uelewa wa kielelezo hicho kwa kuwa kilikuwa katika umiliki wake.

## HABARI KITAIFA

# Mulamula apongeza ushirikiano Marekani, Tanzania

**Na Mwandishi wetu**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Liberata Mulamula, amesema maadhimisho ya miaka 60 ya Shirika la Wafanyakazi wa kujitolea wa Kimarekani la Peace Corps, ni kielelezo na hatua muhimu katika ushirikiano kati ya serikali na watu wa Marekani na nchi hizo.

Mulamula alisema hayo jana wakati wa hafla ya sherehe hizo toka kuwasili kwa wafanyakazi hao kuwasili nchini.

"Maadhimisho ya leo (jana) yanadhihirisha hatua nyingine muhimu katika uhusiano rasmi wa kihistoria na kirafiki baina ya nchi zetu," alisema Mulamula. Alisema aliyekuwa Rais wa Marekani, John F. Kennedy, alianzisha Peace Corps mwaka 1961, akiwapa changamoto vijana wa Kimarekani kuhudumia wanadamu wengine kwa kufanya kazi kwa ajili ya amani na maendeleo katika nchi zingine duniani kote.

"Kwa sababu ya urafiki wa karibu kati ya Kennedy na Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, Tanzania (wakati huo ikiitwa Tanganyika) ilichaguliwa kuwa miongoni mwa nchi za kwanza kabisa duniani kupokea wafanyakazi wa kujitolea wa Peace Corps. Septemba 29, 1961, wafanyakazi wa kujitolea wa Peace Corps wapatao 50 waliwasili Arusha, Tanzania," alisema.

Kwa mujibu wa Waziri Mulamula, takriban wafanyakazi 3,200 wamefanya kazi sambamba na wenzao wa Kitanzania katika mikoa 22 nchini, wakitafuta ufumbuzi utokanao na jamii zao, kutatua matatizo ya elimu, afya, kilimo, mazingira na maendeleo ya vijana.

Alisema wafanyakazi hao wa kujitolea, wamechangia kwa kiasi kikubwa katika maendeleo ya Tanzania.

"Tunatoa shukrani kwa Wamarekani waliofanya kazi bila kuchoka na wafanyakazi wenzao wa Kitanzania katika maeneo ya vijijini kabisa katika nchi yetu wakiwa walimu wa hesabu na sayansi katika shule za sekondari," alisema na kuongeza;

"Wakufunzi wa teknolojia ya habari na mawasiliano, viongozi katika miradi ya kutoa elimu ya afya kwa umma na viongozi katika miradi ya mazingira inayolenga kukidhi mahitaji ya msingi kabisa katika ngazi ya kijiji ya usimamizi endelevu wa maliasili." Awali, Balozi wa Marekani nchini, Donald Wright alisema wafanyakazi hao wanaohudumu nchini walipata mabadiliko chanya kutokana na uzoefu wao huo.

"Baada ya miaka miwili ya kufanya kazi bega kwa bega na wenzao wa Kitanzania wakila pamoja, wakicheka na kujifunza utamaduni wa kila mmoja wao, wafanyakazi wa kujitolea hubadilika milele na huibeba Tanzania mioyoni mwao popote waendapo," alisema Balozi Wright. "Kwa dhati kabisa ninapenda kuwashukuru watu wa Tanzania na serikali katika ngazi zote kwa msaada mkubwa uliotolewa kwa programu na wafanyakazi wa kujitolea katika miaka hii yote. Ninapenda pia kuzishukuru familia na jamii zilizowapokea na kuishi na wafanyakazi wa kujitolea kwa miaka hii yote. Ni kwa sababu yenu, wafanyakazi wa kujitolewa waliweza kujifunza kikamilifu na kunufaika na utamaduni na ukarimu wa Kitanzania," aliongeza.

Alisema kutokana na changamoto za UVIKO-19, kwa sasa hakuna mfanyakazi wa Peace Corps anayehudumu nchini. Awali, Mkurugenzi Mkazi wa Peace Corps nchini, Stephanie Joseph de Goes, alisema kuwa ana matumaini kuwa wafanyakazi wa kujitolea watarejea mwaka 2022.

# Serikali yaonya baa, kumbi kelele za muziki

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imezionya baa na kumbi za starehe, ambazo zimekuwa zikikiuka sheria kwa kushindwa kudhibiti kelele, kwenye shughuli zao kwa kuwa madhara ya kiafya kwa jamii ni makubwa.

Imesema miongoni mwa madhara makubwa ya kiafya yanayosababishwa na kelele za kupindukia ni upungufu wa nguvu za kiume na shinikizo la juu la damu.

Onyo hilo lilitolewa jana, Dar es Salaam na Naibu Waziri Ofisi ya Rais (Muungano na Mazingira), Hamad Chande, wakati akizungumza, kwenye ufunguzi wa mkutano wa wadau wa mazingira.

Mkutano huo uliandaliwa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NECM), kwa ajili ya wamiliki wa kumbi za sterehe, baa na wadau mbalimbali wa muziki kujadili namna ya kudhibiti kelele.

Naibu waziri alisema kabla ya kutoa adhabu kali serikali kupitia NEMC, imekuwa ikikutana na wadau hao kuwaelimisha kuhusu madhara ya kelele, lakini baada ya hapo watakaobainika kukiuka maagizo ya serikali, watachukuliwa hatua za kisheria.

Alisema serikali inathamini mchango wa kumbi za starehe, baa na wadau wa muziki katika ustawi wa jamii, lakini wanaposhindwa kudhibiti kelele zao wanaathiri maisha ya watu wengine kiafya, hivyo serikali haiwezi kuwavumilia. "Ni kweli hayo ni maeneo ya burudani, ambayo watu wetu wanakwenda, kwa ajili ya kuburudika baada ya kazi nyingi, lakini lazima mfuate sheria za nchi," alisema

Aidha, alisema Shirika la Afya Duniani (WHO), kwenye utafiti wake liliwahi kusema kelele ni moja ya vyanzo vya sababu za vifo vya mapema, kutokana na kusababisha sonona na msongo wa mawazo.

Alisema WHO iliwahi kusema pia, kuwa kelele zimekuwa chanzo kikuu cha vifo vya mapema kwa watoto na kwamba kwa mwaka watoto 1,200, duniani hufariki dunia.

Waziri alisema serikali imenza kuchukua hatua kwa kukutana na wizara mbalimbali, ili kuweka mwongozo wa pamoja wa kudhibiti hali hiyo, ambayo wameitamka kuwa ni janga kubwa linalotishia uhai wa watu.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema nia ya kukutana na wadau hao ni kuwaelimisha kuhusu sheria ya mazingira ya mwaka 2004, ili waitii bila shuruti.

Alisema wamekuwa wakifanya msako wa mara kwa mara na kuwakamata wenye kumbi za starehe wanaokiuka sheria hiyo na wengine, wameshawafikisha mahakamani. "Kuna baa, ambazo tayari tumezifikisha mahakamani na kesi zinaendelea, lakini si nia ya NEMC kufika kote huko, ndiyo sababu tunawaita na kuwaelimisha kwanza wajue, kwamba wanachofanya sicho," alisema.







## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Zibuniwe njia zaidi utoaji elimu chanjo ya Uviko-19

**WAKATI** Tanzania ikiendelea kutoa chanjo ya corona kwa watu wake, njia mbalimbali zimeanza kubuniwa kwa ajili ya kuwahamasisha wananchi kujitokeza kuchanja.

Elimu ya uhamasishaji imekuwa ikitolewa na viongozi wa serikali, wanasiasa, viongozi wa dini, vyombo vya habari, wataalamu wa afya na mashirika yasiyo ya kiserikali.

Semina zimekuwa zikitolewa katika maeneo mbalimbali na kuna wakati wahamasishaji wanawafuata wananchi kwenye maeneo ya mikusanyiko kama masoko, magulio na kwingineko.

Tunazipongeza jitihada zinazoendelea za uhamasishaji wa chanjo, lakini tunashauri kwamba ziendelee kubuniwa mbinu zaidi wa kwenda maeneo yenye watu wengi.

Kuna taarifa kwamba watu wa uhamasishaji wa chanjo hiyo mkoani Kigoma wameshauriwa kutumia vijiwe kama vya kahawa kwenda kutoa mada na kujibu maswali yanayowatatiza wananchi kuhusu chanjo.

Ushauri huo ulitolewa wakati wa kikao cha uhamasishaji wa masuala ya chanjo yaliyohusisha makundi mbalimbali wakiwamo waandishi wa habari, viongozi wa dini, wafanyabiashara na makundi mengine.

Mmoja wa washiriki alisema uhamasishaji unaoendelea mkoani humo umekuwa ukiegemea zaidi maeneo ya barabarani pekee, lakini kuna fursa ya utoaji elimu ambayo bado hawajaifanyia kazi.

Alishauri ni vyema yakatumika maeneo yenye mikusanyiko ya kutosha na moja ya eneo hilo ni meza ya duara ambayo hutumiwa na wakazi wa Kigoma kujadili mada mbalimbali za kijamii, kisiasa na michezo.

Mganga Mkuu Mkoa wa Kigoma, Simon Chacha, alisema kila ushauri wenye tija wanaupokea na wanatarajia kufikia maeneo yote ili kuhakikisha kila mtu anapata elimu hiyo na majibu ya maswali yanayomtatiza.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Kamishna wa Polisi, Thobias Andengenye, alisema kuna haja ya kuyatumia makundi ya watu wanao hudumia watu wengi katika ufikishaji wa elimu hasa vijiweni.

Tunauona ushauri kwa wahamasishaji kwenda kutoa elimu vijiweni ambapo watu hukusanyika kwa wingi na pia ni maeneo yenye mijadala kuhusiana na mambo mbalimbali yanayotokea kwenye jamii.

Utaratibu wa wahamasishaji kusikiliza watu na kujibu maswali yanayowatatiza pia ni mzuri kama utatumika kwa sababu ni kweli kwamba kuna mambo mengine ambayo hawayaelewi vizuri kuhusu ugonjwa huo na umuhimu wa chanjo.

Pia upotoshaji unaofanywa na baadhi ya watu ni moja ya mambo ambayo wakati mwingine yanawatatiza wananchi, hivyo kwa kutumia utaratibu wa kujibu maswali ya wananchi, itasaidia kuwapa uelewa na kuona umuhimu wa kuchanja.

Ushauri wetu ni kwa serikali na wadau wengine kutoa sapoti ikiwamo kuwawezesha wahamasishaji ili wayafikie maeneo mengi yenye mikusanyiko mikubwa. Kwa upande mwingine, wahamasishaji wawe wabunifu kuhusu njia za kutumia katika kutoa elimu na kuhamasisha.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Mary Geofrey

# Tumuunge mkono Rais Samia, chanjo ndio mpango mzima

**"MIMI** ni mama, nategemewa kama mama wa watoto wanne, kama bibi wa wajukuu kadhaa, kama mke, kama Rais, kama Amiri Jeshi Mkuu, lakini nimetoka kuonyesha umma wanaonifuata nyuma na nikijua kwamba Rais ni mchungaji nina watu wengi ninaowachunga na wao wananitazama nyuma, kwa hiyo nisingetoka kujihatarishia kifo," alitamka Rais Samia Suluhu Hassan.

Kauli hiyo nzito aliitoa Julai 28, mwaka huu, alipozungumza na viongozi mbalimbali wa serikali, dini na vyombo vya ulinzi na usalama, kabla ya kuzindua huduma ya rasmi chanjo, kukabili virusi vya corona.

Rais Samia alifanya uzinduzi baada ya serikali kupokea chanjo 1,058,400 ya UVIKO-19 aina ya Johnson & Johnson, Julai mwaka huu kutoka Serikali ya Marekani, kupitia mpango wake wa Covax, unaolenga kusaidia nchi zinazoendelea katika kukabiliana na janga hilo.

Rais Samia alisema, hawezi kuhatarisha maisha yake huku akijua anaongoza kundi kubwa la watu wanaomtegemea, akiwa kama Rais, Amiri Jeshi Mkuu, Mchungaji wa Watanzania, Mama, Bibi na Mke.

Alisisitiza kuwa amekubali kwa hiari yake kuchanja, akitambua kuwa alishachanja chanjo tano kadhaa ndani ya mwili wake, ambazo anaendelea kuishi nazo kwa miaka 61 bila ya madhara yoyote.

Alisema haoni hatari ya kuchanja ilhali wanasayansi wa nje na ndani ya nchi wameshajiridhisha kuwa chanjo hiyo ni salama.

Kadhalika alisema kwa Watanzania ambao familia zao hazijakumbwa na ugonjwa huo ni rahisi kupinga chanjo hiyo, lakini kwa wale walioguswa wanatamani kuchanjwa haraka.

Aliwaomba Watanzania wasivunjane moyo bali kuendelea kutiana moyo katika kukabiliana na janga hilo lililoikumba dunia.

Septemba 23, mwaka huu, Rais Samia akihutubia Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, aliwakikishia kuwa uongozi wake, Tanzania itaendelea kuwa mstari wa mbele katika kushirikiana na mataifa na wadau wengine duniani kutatua changamoto zinazoukabili ulimwengu.

Katika hotuba hiyo, Rais Samia alieleza kuwa ugonjwa wa UVIKO-19 bado unaendelea kupunguza kasi ya kufanikisha Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) katika muda uliopangwa na kwamba kwenye baadhi ya nyanja, taarifa zinaonyesha kuwapo athari zilizorudisha nyuma mafanikio yaliyopatikana.

Rais Samia alitoa mfano takriban watu milioni 71 duniani wanatarajiwa kurejea katika umaskini, licha ya kwamba walikwishaondokana nayo. Hapo anasisitiza kuwa iko haja ya kuunganisha juhudi kubadili hali hiyo, hasa kwa kuwa changamoto za janga hilo hazijali hali ya nchi ilivyo.

Aidha, Rais Samia alizishukuru Taasisi za Kimataifa likiwamo Shirika la Fedha Duniani (IMF) kwa jitihada zao za kusaidia nchi zinazoendelea ikiwamo Tanzania zisiathirike zaidi kiuchumi.

Vilevile, alieleza Tanzania inachukua hatua mbalimbali kukabiliana na Uviko-19 na wiki hii, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, alisema kila wiki wanawasilisha ripoti ya maradhi hayo kwa Shirika la Afya Duniani (WHO) na hadi Septemba 27 mwaka huu, waliochanjwa walishafika 400,000 kati ya chanjo milioni moja.

Ni wazi kuwa Watanzania tunapaswa kumuunga mkono Rais Samia kwa kuhikikisha tunatafuta maarifa ya kutosha kuhusu usalama wa chanjo kupitia vyombo sahihi ili kupata chanjo.

Tusisubiri ndugu, jamaa na marafiki wapoteze maisha ndipo tumiminike kwenda kuwahi chanjo. Hii ni fursa muhimu kwa Watanzania wote na tusikubali kuipoteza.

Ni muhimu pia kuachana na maneno ya mitaani kuhusu chanjo hiyo kwa sababu taarifa hizo siyo za wataalamu ni watu wanaojaribu kuzielezea kwa kufikiri kwao. Tujiulize swali dogo tunafahamu kina cha upeo wa kufikiri kwao? Je, wana ulinganifu wa uelewa wa serikali, inayotuambia tuchanje?

Mtaalamu wa Afya na viongozi wa serikali ndio wanaoweza kueleza suala hili kwa kina na watu wakapata elimu sahihi ya kumpa mwelekeo wa maamuzi ya kuchukua.

Tusichukulie mizaha suala la kitaifa ambalo limepoteza ndugu, jamaa na marafiki zetu lakini pia limeturudisha nyuma kiuchumi.

Na siyo tu Tanzania iliyoathirika ni dunia na tumeshuhudia Rais na viongozi wengine wa nchi wakiwahi kupata chanjo ni wazi kuwa hakuna mtu anayeweza kuhatarisha maisha yake binafsi na taifa lake.

Rais Samia, ameshachanja na ameshatoa maelekezo elimu itolewe, chanjo bado zipo tuendelee kupata chanjo kwa sababu tushaambiwa hazina madhara na tumeshuhudia waliochanja hawajapata madhara yoyote.

## HABARI KITAIFA

# DAWASA kusajili magari huduma binafsi majitaka

**Na Frank Monyo**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) imetangaza kufanya usajili kwa watoa huduma binafsi wa magari na kutoa vibali vya uendeshaji kuanzia (leo) Oktoba Mosi hadi 16, 2021.

Meneja Uhusiano kwa Umma wa mamlaka hiyo, Everlasting Lyaro, alisema lengo la usajili huo ni kuratibu huduma ya majitaka kupitia magari na kuhakikisha majitaka yote yanayonyonywa yanamwagwa kwenye mabwawa ya kutibu majitaka yanayomilikiwa na DAWASA.

"Zoezi hili litafanyika katika mabwawa ya majitaka Vingunguti Dar es Salaam kuanzia leo (jana) hadi Oktoba 16, 2021) ambapo magari yatakayosajiliwa yatabandikwa stika za DAWASA na kupewa cheti cha usajili kuonyesha kuwa wamekidhi vigezo vya kutoa huduma hiyo kwa jamii," alisema na kuongeza kuwa:

"Madereva wa magari ya majitaka wanatakiwa kufika na magari yao wakiwa na picha mbili za rangi za mmiliki wa gari pamoja na nakala ya kitambulisho chake (kura, utaifa au hati ya kusafiria), nakala ya kadi ya gari, nakala ya bima na nakala ya leseni ya dereva vilivyothibitishwa na mwanasheria na nakala ya Wakala wa Vipimo (WMA) inayothibitisha ujazo wa tangi."

Aliongeza kuwa usajili wa magari ni moja ya mkakati wa kutoa huduma bora ya majisafi na majitaka kwa wananchi ili kukabiliana na changamoto zozote zitakazoweza kujitokeza hasa magonjwa.



Diwani wa Kata ya Kijitonyama, Mhandisi Damas Samora (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, baada ya kuzindua kituo cha huduma kwa wateja na mauzo cha kampuni ya vifaa vya umeme wa jua ya D.Light, eneo la Makumbusho, mkoani Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa D.Light Tanzania, Charles Natai na Meneja Biashara wa kampuni hiyo, Kanda ya Pwani, Gasper Mrosso. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Madiwani wambana DED madeni ya watumishi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA.

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Ushetu, mkoani Shinyanga, limemtaka Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Mwalimu Lino Mwageni, kulipa madeni ya watumishi yanayofikia Sh. bilioni 1.6.

Wamesema hatua hiyo, itasaidia kuondoa hoja za wakaguzi na kupata hati safi mwaka wa fedha ujao.

Madeni hayo ni kuanzia mwaka wa fedha 2019/20, mpaka mwaka wa fedha 2020/21 na fedha hizo zinatokana na madeni ya nauli kwa watumishi kwenda likizo na uhamisho kutoka kituo kimoja kwenda kingine.

Diwani wa Nyankende, Doa Limbu, aliyabainisha hayo jana wakati akichangia taarifa ya ufungaji wa hesabu za mwaka wa fedha 2020/21, ulioishia Juni 30 katika mkutano maalumu wa baraza la madiwani. Alisema mkurugenzi anatakiwa kuhakikisha watumishi wake, wanalipwa stahiki zao kwa wakati.

Alisema mwaka wa fedha 2019/20 watumishi wa halmashauri hiyo, walikuwa wakidai Sh. bilioni 1.4, lakini kwa sasa zimeongezeka mpaka kufikia Sh. bilioni 1.6 kwa mwaka wa fedha 2020/21 na inavyoonekana zitazidi kuongezeka, kila mwaka.

Aidha Limbu alisema moja ya sababu za madeni hayo kuongezeka kila mwaka ni ofisi ya mkurugenzi kutokumaliza kulipa madeni hayo ya watumishi, ikiwamo fedha za uhamisho kulinganisha na fedha za nauli za likizo.

"Halmashauri yetu ina vigezo vya kulipa madeni haya na kutokuyalipa kwa wakati yanafanya halmashauri kutokuwa na afya na hii itakuwa moja ya sababu ya kuendelea kupata hati, yenye mashaka kama tusipolitatua kwa wakati tatizo hili," alisema Limbu.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Gagi Lala, alisema katika kikao hicho wanajadili uhalali wa madeni hayo na atahakikisha anasimamia, ili yalipwe kwa wakati.

Naye Mkurugenzi Mwageni, alikiri kuwapo madeni hayo ndani ya ofisi yake, hivyo muda wowote vikao vya bajeti vitaanza kukaa na

# Naibu Waziri ataka kasi utoaji hati

**Na Hassan Mabuye,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amewataka watumishi wa sekta ya ardhi, Mkoa wa Dodoma kuongeza kasi ya uandaaji na utoaji hatimiliki za ardhi kwa wananchi.

Dk. Mabula alitoa agizo hilo mwanzoni mwa wiki hii, alipokutana na viongozi na watendaji wa sekta ya ardhi katika halmashauri za wilaya za Kondoa, Chemba, Bahi na Chamwino katika ziara yake ya kukagua maendeleo ya sekta hiyo.

Alielekeza kuwa, kila ofisi ya halmashauri katika Mkoa wa Dodoma kuandaa na kutoa angalau hatimiliki za ardhi 100, kila mwezi kwa kuwa kuna baadhi ya halmashauri, ambazo amezitembelea na amekuta zinatoa zaidi ya hatimiliki 300 kwa mwezi.

"Huwezi kuwa na lengo la kuandaa hati 120 kwa mwaka. Haiwezekani hata kama kungekuwa na mtumishi mmoja. Nendeni mkapitie upya malengo yenu, labda mgeniambia haya ni malengo ya miezi mitatu sawa, lakini si malengo ya mwaka mzima," alisema.

Naibu Waziri Mabula alitoa muda wa hadi Oktoba 21, mwaka huu, halmashauri hizo, zijipange kuanza kuoa elimu kwa wananchi kuhusu faida za umiliki wa ardhi kwa hati na amemuagiza Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Dodoma, kufuatilia kwa karibu.

Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Dodoma, Thadei Kabonge, aliwataka watumishi wa sekta ya ardhi mkoa, kuepuka kuzalisha migogoro mipya hasa, ile ambayo inazalishwa kwa uzembe na watumishi wenyewe kwa kuwa inachangia katika kuchelewesha umilikishaji wa ardhi kwa wananchi.

Katika hatua nyingine, Ofisa Utumishi kutoka Ofisi ya Kamishna wa Ardhi Msaidizi, Mkoa wa Dodoma, Swaumu Muganyizi, aliwataka watumishi wa sekta ya ardhi kuwa waadilifu na kuboresha utoaji huduma kwa wananchi na kuepuka rushwa hasa katika umilikishaji.

# Kesi ya Mkurugenzi Temeke Okt. 19

**Na Kulwa Mzee**

KESI inayomkabili aliyekuwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke, Lusubilo Mwakabibi na Mratibu wa Mradi wa Uendelezaji Jiji la Dar es Salaam (DMDP), Edward Haule, imeahirishwa hadi Oktoba 19, mwaka huu.

Kesi hiyo ya matumizi mabaya ya ofisi na madaraka ilitajwa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Evodia Kyaruzi.

Wakili wa Serikali, Sylvia Mitanto, alidai upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika na kuomba shauri liahirishwe hadi tarehe nyingine itakayopangwa.

Mahakama ilikubali kuahirisha hadi Oktoba 19, mwaka huu kwa ajili ya kutajwa na washtakiwa wataendelea kuwa nje kwa dhamana.

Washtakiwa hao walifikishwa mahakamani kwa mara ya kwanza, Agosti 20, 2021 na kusomewa kesi ya uhujumu uchumi na shtaka la kwanza ni matumizi mabaya ya ofisi, wanadaiwa kutenda kosa hilo kati ya Machi 2020 na Machi 2021 katika Manispaa ya Temeke.

Inadaiwa siku hiyo ya tukio, Mwakabibi akiwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke na Haule akiwa Mratibu wa Mradi wa DMDP, wakiwa waajiriwa wa manispaa hiyo, katika utekelezaji wa ardhi walielekeza ujenzi wa stendi ya mabasi eneo la Buza, kiwanja ambacho kinamilikiwa na Dayosisi ya Kanisa la Anglikana, bila kuwa na ruhusa.

Shtaka la pili ni matumizi mabaya ya madaraka, linaodai Machi 2020 na Machi 2021 katika eneo hilo, washtakiwa kwa makusudi walitumia madaraka yao vibaya kinyume na kifungu cha 3(1) cha Sheria ya Ardhi na kifungu cha 3,4,5,7 na 11 cha Sheria ya Ardhi ya mwaka 2019.

# TBL yazindua chanjo corona kwa wafanyakazi

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bia Tanzania (TBL), imeunga mkono jitihada za serikali za kuhamasisha kampeni ya chanjo, dhidi ya UVIKO-19, ambapo jana ilizindua chanjo katika kiwanda cha Dar es Salaam.

Chanjo ya UVIKO-19 iko wazi kwa wafanyakazi wote, familia zao na wakazi wanaoishi maeneo ya jirani na jamii na kiwanda. TBL imeajiri jumla ya wafanyakazi 1,300 katika viwanda vyake vitano, vilivyopo katika mikoa mbalimbali.

Uzinduzi wa Dar es Salaam uliongozwa na Katibu wa Afya wa Mkoa, Sister Mathew, aliyemwakilisha Mganga Mkuu wa Mkoa, Dk. Rashid Mfaume, na kuhudhuriwa na Mkurugenzi Mtendaji wa TBL, Jose Moran na Mkurugenzi wa rasilimali watu, Rabina Masanja.

Moran alisema: "Chanjo kwa ujumla ni njia salama na bora ya kuzuia magonjwa na kuokoa maisha. Chanjo pia hupunguza kuenea kwa maambukizi, ambayo inamaanisha kwamba wakati tunapata chanjo, hatujilindi tu, bali tunalinda pia wale wanaotuzunguka.

"Chanjo ni nafasi yetu nzuri ya kujilinda sisi wenyewe, familia zetu na wenzetu kutokana na hatari za UVIKO-19 na tunaamini kuwa watu wengi iwezekanavyo watatumia fursa hii, kwani tutakuwa tunatoa huduma hii kwa jamii zetu pana."

Kwa upande wake, Masanja alisisitiza kwamba afya na usalama wa wafanyakazi wao ndio kipaumbele chao cha kwanza na kwamba ndio maana wameshirikiana na Wizara ya Afya kuhakikisha kuwa, wafanyakazi wao wote na familia zao wamepewa chanjo, kwenye maeneo yao yote ya kazi. "Hii sio tu itasaidia kukuza usalama kwa kila mtu , pia itahakikisha mwendelezo wa biashara, alisema Masanja.

Zoezi la chanjo la TBL litaendelea hadi leo katika viwanda vyote vya TBL vilivyopo Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya na Arusha.



Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa TBL PLC, Jose Moran (katikati), akizungumza na Katibu wa Afya wa Mkoa wa Dar es Salaam, Sister Mathew (kulia), wakati wa uzinduzi wa zoezi la chanjo ya Covid-19 kwa wafanyakazi wa kampuni na wakazi wa maeneo yanayozunguka viwanda vyake, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa Rasilimali Watu wa TBL, Rabina Masanja, Mkurugenzi wa Mawasiliano na Uhusiano, Mesiya Mwangoka na Mratibu wa Chanjo mkoa, Juma Haule. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC aangukia wazee malezi vijana

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, amewataka wazee wa mkoa huo, kutafuta namna ya kuwalea vijana wao, ili wakue katika maadili mazuri na kujikita kufanya kazi kwa bidii.

Kunenge aliyasema hayo jana, wakati wa kikao cha uundaji wa Baraza la Wazee kilichofanyika mjini hapa.

Alisema wazee watakapowajibika vizuri kwenye eneo la malezi, watachangia vijana kuwa na mabadiliko kwa kufanya kazi mbalimbali wanazopata, kwenye kampuni zinazowekeza katika mkoa.

"Wazee mtakuwa washauri wangu, tumejipanga kubadilisha maisha ya Mkoa wa Pwani kwa kushirikiana na nyie na tutafanikiwa," alisema.

Alisema kuna malalamiko kutoka kwa baadhi ya wawekezaji yakilenga vijana, ambao wanapata ajira, lakini wanapopata malipo hawaonekani sehemu zao za kazi hali, ambayo inapoteza uaminifu kwa wakazi wa mkoa.

"Kwa kushirikiana na nyie tunataka vijana wabadilike. Tuone namna ya kuwasaidia, ili wabadilike kwenye maeneo wanayopata kazi. Bila kufanya hivyo idadi ya wanaoajiriwa watachukuliwa kutoka mikoa mingine jambo ambalo si jema," alisisitiza.

Kunenge pia, alizielekeza halmashauri kuhakikisha kila kituo (hospitali na vituo vya afya) cha kutolea huduma za kinakuwa na chumba maalumu, kwa ajili ya huduma za Wazee.

Pia alisema Kutokana na uhaba wa vyumba vya kutolea huduma na uchache wa wataalam kwa baadhi ya zahanati, umewekwa utaratibu wa kuhakikisha, kila mzee anahudumiwa.

Akitoa taarifa kwa mkuu wa mkoa, Katibu Tawala Msaidizi upande wa afya, Dk. Gunini Kamba, alisema pamoja na kushirikiana na wadau katika kutoa huduma, bado kuna vikwazo wanakabiliwa navyo ikiwamo uchache wa maofisa ustawi wa jamii katika halmashauri.

Kikwazo kingine, kwa mujibu wa Dk. Komba, ni ukosefu wa madaktari bingwa wa magonjwa ya wazee, ukosefu wa wadau katika eneo la wazee na ufinyu wa bajeti za masuala ya wazee na huduma za ustawi wa jamii ngazi za halmashauri.

Aidha, alibainisha kuwa kuna mikakati ya kuboresha huduma na kuinua hali za wazee kwa kuwatambua hasa wale, wasiojiweza na wategemezi wao.

Mikakati mingine, alisema ni pamoja na kuhakikisha halmashauri zinaendelea kufanya utambuzi wa wazee na kuweka utaratibu kwa wazee wasio na uwezo kupatiwa kadi za matibabu.

HABARI KITAIFA

## Tigo, Infinix waleta Infinix Zero X PRO

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Tigo Tanzania imeshirikiana na Infinix Tanzania kuzindua simu janja toleo jipya yenye kiwango cha juu ya 108MP na 60x kamera, ijulikanayo kama Infinix ZERO X PRO.

Imebainishwa kwamba simu hiyo itauzwa kuanzia Sh. 800,000.

Akizungumza wakati wa kutangaza simu hiyo Mkuu wa Kitengo cha maduka na bidhaa za intaneti Tigo Tanzania, Mkumbo Myonga, alisema:

"Ushirikiano wa Tigo na Infinix Tanzania unaonyesha zaidi lengo la kuunganisha nguvu na kuwa vinara katika utoaji wa huduma za kidigitali Tanzania, kwa kuongeza upatikanaji wa simu bora sokoni zitakazochochea kuongezeka kwa huduma za Kidigitali."

Myonga pia aliongeza kuwa kuzindua Infinix Zero X PRO kunadhiirisha kwamba wateja wa Tigo watajipatia kilicho bora, suala litakalochangia kuongeza thamani ya mazingira ya kibiashara nchini.

Kwa mujibu wa Myonga, simu hizo zinapatikana katika maduka yote ya Tigo nchini kote na zitakua na Ofa ya GB 96 za Intaneti Bure kutumia mwaka mzima.

Ofisa Uhusiano wa Infinix, Aisha Karupa, alisema kutangazwa kwa toleo jipya la simu ya Infinix zero x pro kunadhihirisha maana halisi ya teknolojia, maana inahusisha uvumbuzi wa bidhaa mpya na kuvuka mipaka zaidi na zaidi. Alisema ili kuwafikia wateja kiurahisi na Infinix ZERO X pro inamwezesha mtumiaji kufanya vitu vingi kwa pamoja maana ina processor ya Helio

## Lindi, Ruvuma zapewa pikipiki kulinda misitu

**Na, Said Hamdani,** LINDI

KATIKA kuhakikisha misitu inaendelea kulindwa, Programu ya mnyororo wa thamani mazao ya misiti (FORVAC) imeipa mikoa ya Lindi na Ruvuma vitendea kazi vitakavyotumiwa na ma ofisa mali asili na kamati za vijiji ili kuboresha na kulinda mazao hayo.

Vitendea kazi hivyo ni pikipiki 15 aina ya Yamaha za thamani ya Sh. 90,000,000 zimekabidhiwa kwa viongozi wa mikoa hiyo, ambapo Lindi umekabidhiwa nane na saba zilizobaki umepewa Ruvuma.

FORVAC inatekeleza shughuli zake vijiji 103 vilivyopo katika wilaya 12 kwa mikoa mitano ya Lindi, Tanga, Ruvuma, Dodoma na Manyara.

Wilaya zinazohusika na programu hiyo ni Nachingwea, Liwale na Ruangwa (Mkoa wa Lindi), Tunduru, Namtumbo, Songea, Nyasa na Mbinga (Ruvuma), Handeni na Kilindi (Tanga), Kiteto (Manyara) na Mpwapwa (Dodoma).

Mwakilishi wa Balozi wa Finland, anayeshughulikia maliasili, Heini Vihemaki, alisema msaada huo ni utekelezaji wa uhusiano mzuri kwa nchi hizo mbili.

# Mabinti, mama wanolewa kuhusu mabadiliko tabia

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

ZAIDI ya mabinti balehe na kinamama vijana 84,000 nchini wenye umri wa miaka 17 hadi 24 wamepewa elimu ya mabadiliko ya tabia, kwa ajili ya kujikwamua kiuchumi kama sehemu ya kupambana dhidi ya maambukizi mapya ya VVU/Ukimwi.

Elimu hiyo ilitolewa na Shirika lisilo la kiserikali la FHI360, kwenye mradi wa Epic unaotekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano kwa ufadhili wa mpango wa dharura wa Rais wa Marekani wa kukabiliana na UKIMWI (PEPFAR) na Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID), uliojikita kufikia na kuendeleza udhibiti wa janga la VVU/Ukimwi hapa nchini.

Hayo yalibainishwa jana na Ofisa Mabinti Balehe na Kinamama vijana kutoka shirika hilo, Agnes Junga, alipowatembelea baadhi ya mabinti 30 wanaoendelea kupata ujuzi katika Chuo cha St. Francis Vocation Training Center (SFS VTC), kilichopo kata ya Mwakata Halmashauri ya Msalala.

Alisema kuwa hadi sasa wamewafikia mabinti balehe na kinamama vijana 84,000 na kuwapatia ujuzi mbalimbali na tabia hatarishi, kati ya hao vijana 56,000 wamewezeshwa kiuchumi na kwamba kati yao 13,000 wameshaanzisha biashara zao na kuendesha maisha.

"Katika chuo hiki tuna mabinti balehe na kinamama vijana 30 wanaosoma fani tofauti ikiwemo umeme, ufundi magari, kompyuta, ufundi cherehani na saluni, lengo la mradi huu ni kuwakinga na maambukizi mapya ya VVU na UKIMWI vijana hawa,"alisema Junga.

Aliongeza kuwa"Tunatoa elimu hii kwa mabinti balehe na wanawake vijana wenye umri kati ya miaka tisa hadi 24, wanaoishi katika mazingira hatarishi na wanafanya ngono katika umri mdogo ili waweze kumudu gharama za maisha.

Kwa upande wake, Mratibu wa Mafunzo hayo kutoka katika chuo hicho, Charles Maganga amelipongeza shirika la FHI 360 kwa kuona umuhimu wa kuthamini watoto wa kike na kuwapeleka chuoni kupata mafunzo ambayo yatawasaidia katika maisha yao ya baadae.

Alisema kwa ujunzi wanaowapatia mabinti hao watakuwa na uwezo wa kufanyakazi popote iwe kwenye sekta binafsi au serikali kupitia fani ya Umeme, Uchomeleaji na ufundi magari, udereva, Kompyuta, ufundi cherehani, saluni na mapambo.

Mmoja wa wanufaika wa mradi huo, Ester Obadia alisema walichaguliwa kujiunga na masomo chuoni humo kupitia vikundi vya wasichana vinavyosimamiwa na Shirika la FHI 360 na wanatarajia kutumia mafunzo hayo kwa ajili ya kujiari na kujiingizia vipato.

Naye, Mary Edward alisema awali waliishi katika mazingira magumu na kusababisha kuingia kwenye tabia ambazo zilikuwa zikihatarisha maisha yao, lakini kwa mafunzo hayo yatawasaidia kujitegemea na kujiepusha kujiingiza kwenye vishawishi vinavyoweza kuwaingiza kwenye mazingira hatarishi ya ngono.




Mkuu wa Kitengo cha Maduka na Bidhaa za Intaneti wa Tigo, Mkumbo Myonga, akizungumza jijini Dar es Salaam jana, katika uzinduzi wa simu janja ya Infinix Zero X PRO. Kulia ni Ofisa Uhusiano wa Infinix Tanzania, Aisha Karupa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wagonjwa wa moyo watakiwa kufuatilia matibabu

**Na Romana Mallya**

DAKTARI Bingwa wa Magonjwa ya Moyo wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Tulizo Sanga, amewataka wagonjwa wa moyo wafuatilie matibabu kwa makini hasa kipindi hiki cha corona.

Amesema wagonjwa hao wako katika kundi, ambalo likiupata ugonjwa huo, huwekwa kwenye oksijeni na chumba cha wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalum (ICU).

Dk. Sanga aliyasema hayo jana, katika Siku ya Moyo Duniani, ambayo JKCI iliwafikia wananchi wa Kigamboni na kutoa huduma ya upimaji wa magonjwa ya moyo katika Hospitali ya Wilaya ya Kigamboni.

Akizungumza katika siku hiyo, Dk. Sanga alisema dunia inakabiliwa na janga la corona na waathirika wa shida za moyo, sukari na magonjwa mengine wamekuwa wakipata aina mbaya ya ugonjwa.

"Wako kwenye kundi la watu ambao ni rahisi kupata ugonjwa wa corona na vile vile hawa ni wale ambao wanapata ugonjwa ambao ni mbaya. Wengi huhitaji kuwekwa kwenye oksijeni na kutibiwa katika vyumba vya wagonjwa mahututi (ICU) ni miongoni mwa wagonjwa wengi, ambao wanaugua ugonjwa huo."

Alisema chanjo ya corona imepatikana na watu wameanza kuchanja baada ya Rais Samia Suluhu Hassan, kuanzisha uchanjaji na kuwaomba wananchi wafanye utaratibu wa kuipata.

"Utafiti umeonyesha chanjo inapunguza makali ya ugonjwa wa corona, sisi wahanga wa moyo, ambao tunaweza kupata ugonjwa huu kirahisi tunashauriwa wote tupate chanjo ya corona, ili hata kama inatupata tusipate aina mbaya ya ugonjwa na hatimaye kifo," alisema.

Alisema siku ya moyo duniani ni maalum, kwa ajili ya kukumbusha jamii kuwa shida za moyo zipo duniani kwa kiasi kikubwa.

"Shida za moyo duniani zinaongoza kwa vifo, kuwafanya watu wasiweze kukaa, kufanya kazi waishi kwa kuwa tegemezi, kwa sababu ya madhara ya shida za moyo zinazosababisha.

Aliyataja madhara hayo kuwa ni kiharusi, shida za figo na macho, ambayo chanzo huwa ni moyo, ambao gharama zake za matibabu huwa kubwa. Alisema wanatumia siku hiyo kwa kuelimisha jamii, njia bora za kuepukana na kadhia hiyo.

"Bahati nzuri magonjwa ya moyo yanazuilika hata kama umegundulika una shida utatibiwa kwa kufuata utaratibu, njia za kuzuia yasikupate ni kula chakula vizuri, kupunguza wanga kwenye vyakula, sukari, mafuta na kuongeza viwango vya mboga za majani na vitamini mbalimbali na kufanya mazoezi," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Fatma Nyangasa, aliwahamasisha wananchi wake kujitokeza, kupima afya zao.

Kuhusu chanjo alisema Kigamboni wana jukumu la kuelimisha na kuhamaisha wananchi mitaani na ambao wako tayari wanachanjwa.

Mzee Crosteri Turubera, ambaye amepimwa katika maadhimisho hayo ya moyo na kupewa dawa, aliwaomba wananchi wajitokeze wapime na kujua maendeleo ya afya zao.

# TGNP yawanoa madiwani bajeti mrengo wa kijinsia

Na Yasmine Protace

MTANDAO wa Jinsia Tanzania (TGNP) umetoa mafunzo ya bajeti yenye mrengo wa kijinsia kwa madiwani wa Halmashauri Ubungo, mkoani Dar es Salaam pamoja na watendaji kata na wenyeviti wa halmashauri ya hiyo.

Akifungua mafunzo hayo ya siku mbili Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP Mtandao, Lilian Liundi, alisema mafunzo hayo lengo lake ni kuwajengea uelewa kwa viongozi na wanajamii juu ya umuhimu wa kupanga mipango na bajeti kwa mrengo wa kijinsia.

Aliongeza kuwa mafunzo hayo yatawasaidia kushirikishana uzoefu kuhusu umuhimu wa wanajamii, kushirikiana na viongozi wa serikali katika kushughulikia changamoto katika kata zao.

"Mafunzo hayo yatawasaidia kupitia na kuchambua mipango na bajeti katika ngazi ya kata na halmashauri kwa mrengo wa kijinsia," alisema Liundi.

Aliongeza kuwa mafunzo hayo yatawasaidia kupanga mipango wa utekelezaji wa masuala aliyojifunza. Mkufunzi wa mafunzo hayo, Deo Temba, ambaye ni mwanaharakati wa masuala ya kijinsia, alisema jamii inatakiwa kufahamu umuhimu wa bajeti yenye mrengo wa kijinsia.

Alisema kuwa majukumu ya kijinsia yasimkandamize mwanamke.

Diwani Viti Maalumu Ubungo, Leberata Samson, alisema kuwa mafunzo hayo yatawajengea uwezo juu ya bajeti yenye mrengo wa kijinsia.

Alisema mafunzo hayo yatamwezesha kuitetea bajeti yenye mrengo wa kijinsia.

"Mafunzo haya yamenisaidia kujua vitu vingi, hivyo katika mwaka wa fedha nitaomba utaratibu ufanyike ili katika shule zetu za msingi na sekondari tuongezewe idadi ya matundu ya vyoo," alisema. Aliongeza kuwa kutokana na kuwapo kwa idadi kubwa ya wanafunzi wa kike katika shule za msingi na sekondari katika bajeti tutahakikisha inaandaliwa kimrengo wa kijinsia ili wanawake waepukane na changamoto ya kurundikana katika vyoo vyenye matundu machache.

Aliongeza kuwa watahakikisha maji yanapatikana katika vyoo vya wanafunzi wa kike.

Neema Abed, Mtendaji wa Kata ya Upendo Kimara, Dar es Salaam, alisema kuwa alikuwa hajui maana ya usawa wa kijinsia, bajeti ya mrengo wa kijinsia, mawazo mgando, lakini baada ya mafunzo hayo ataenda kuwaelimisha wanajamii.

William Chitanda, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa Kimara Matangini, alisema kuwa mafunzo hayo ni mara yake ya kwanza kuyapata, na kwamba yatamsaidia katika kazi zake ikiwamo na kuandaa bajeti kwa mrengo wa kijinsia.




Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi, akizungumza wakati wa uzinduzi wa huduma mpya ya Wekeza Akaunti, jijini Dar es Salaam juzi. Kushoto ni Meneja Mwandamizi Idara ya Bidhaa, Janet Rwegasila na Mkuu wa Idara ya Bidhaa wa Benki ya NMB, Aloyse Maro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Huduma fedha kidigitali zatajwa kuleta tumaini

Na Mwandishi wetu

MATUMIZI ya huduma kidigitali yameleta mapinduzi ya mifumo kwenye sekta mbalimbali nchini na maisha ya watu kwa ujumla, imeelezwa.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Letshego's Group, Andrew Okai, aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maendeleo ya kidigitali kwenye sekta ya fedha katika kubuni njia sahihi zitakazowezesha upatikanaji wa huduma kwa urahisi.

Alisema utaratibu huo utamwezesha mtumiaji kupata huduma za taarifa mbalimbali za mikopo, kufanya miamala na huduma nyingine za kifedha kwa haraka.

Alisema "kutokana na changamoto kadhaa kama ugonjwa wa UVIKO 19 kwa sasa kuna uhitaji wa kuja na mikakati kama hii ya kushughulikia huduma za kibenki kwa njia ya kidigitali, ili kuwawezesha wateja kutosongamana wakati wa kupata huduma,"alisema na kuongeza;

"Kwa sasa wanaweza kupata huduma kwa njia ya simu zao za mkononi au televisheni na tena wakanufaika kwa haraka na ufanisi zaidi huku wakiwa wamejilinda na ndiyo maana Letshego imekuwa karibu zaidi kuwahudumia wateja wake kiubunifu."

Alisema benki hiyo itaendelea na utamaduni wake wa kutumia zaidi matumizi ya mifumo ya kidigitali hasa huduma ya LetsGo katika kuwaunganisha wateja wake, ili waendelee kufurahia huduma.

Alisema: "Kwa sasa LetsGO platform inaweza kupatikana kupitia simu ya mkononi na tovuti na kwamba mteja ataweza moja kwa moja kuingia kwenye akaunti yake na kuendelea kujipatia huduma kama za mikopo, taarifa mbalimbali na huduma nyinginezo kwa Botswana na Nigeria.".

Afisa Mtendaji Mkuu wa Letshego Tanzania, Andrew Tarimo, alibainisha kuwa muda mfupi ujao wateja wa taasisi hiyo hapa nchini wataanza kunufaika na ubunifu huo wa kidigitali wa kupitia huduma ya Lets Go ambayo itawaunganisha na wateja wengine Afrika.

# Akaunti ya Wekeza NMB kuimarisha uwekezaji akiba

Na Mwandishi Wetu

BENKI ya NMB Iimezindua akaunti ya dhamana ya muda mrefu, inayoambatana na bima ya maisha bure.

Akaunti hiyo iliyopewa jina la 'Wekeza' ni ya kwanza katika soko nchini. Akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Mkuu wa Biashara na Wateja Binafsi, Filbert Mponzi, alisema Akaunti ya Wekeza itavutia kwa maana ina kiwango cha riba hadi kufikia asilimia 12 kwa ambao watakuwa na uwekezaji wa muda mrefu.

Alibainisha kiwango cha riba kitakwenda sambamba na idadi ya miaka ambayo mteja anataka kuwekeza.

"Tumeamua kuja na ubunifu huu kama ilivyo kawaida yetu, lengo ni kuwafundisha Watanzania utamaduni wa kuweka akiba, ndiyo maana tumeruhusu kutoa fedha, kwenye akaunti hiyo mara mbili kwa mwaka, Juni na Disemba, kwa sababu tunafahamu huenda ikatokea dharura au kulipia ada za watoto," alisema Mponzi.


Mponzia alisema: "Mtakumbuka hivi karibuni benki yetu ilipata tuzo sita za kimataifa mojawapo kutoka jarida la 'International Banker' Benki ya NMB imekuwa benki bora kwa ubunifu wa bidhaa kwa wateja binafsi.

"Tunafurahia kumudu kuwapa wateja wetu njia nyingine salama na ya muda mrefu kuhifadhi fedha, ikumbukwe tunatoa huduma katika mazingira shindani zaidi, lakini kwa mara nyingine tunathibitisha kuwa tunaweza kuendelea kuleta bidhaa mpya, zinazoongeza thamani kwa wateja.

"Tunajivunia zaidi huduma yetu ya Wekeza, tumejipanga kuhakikisha tunaongeza fursa kwa wateja wetu, wakati tunaendelea kuwatia moyo kujizoesha utaratibu mzuri wa matumizi ya fedha."

Awali Mkuu wa Idara ya Bidhaa, Aloyce Maro alisema Akaunti ya Wekeza inatoa fursa kwa mteja kuanza kwa kuweka kiasi cha Sh. 250,000, ambapo ataanza kwa kupata riba ya asilimia mbili, kila baada ya miezi sita.

"Mteja atapata nafasi ya kuendelea kuweka akiba katika akaunti yake kadiri awezavyo, ambapo riba itaongezeka kulingana na kiasi alichonacho. Vilevile kutakuwa na huduma ya bima ya maisha bure itakayotolewa kulingana na kiasi cha akiba iliyopo hadi kufikia Sh. Milioni 50, itawahusu wateja waliopata kilema cha maisha au kifo," alisema Maro.




Ukurasa 14

Uviko-19, Wamachinga wasitugombanishe





# BUFE

IJUMAA OKTOBA 1, 2021

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA


## KILELE SIKU YA WAZEE DUNIANI
## Tanzania imeshafikia mengi ya kujivunia?

Ukurasa 12

# TARI yafungua kituo Dodoma kuweka sawa uzalishaji shambani Kanda Kati

- Waziri Mkenda: Jiandaeni kwa mapya
- Mkurugenzi: Tumejipanga, tunakuja

**Na Elizabeth Zaya, aliyekuwa Dodoma**

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), miongoni mwa shughuli zake inazofanya ni utafiti kwa ajili ya kuendeleza, kuinua na kutoa mchango katika kuboresha sekta ya kilimo nchini, ili ilete tija.

Hivi karibuni asasi hiyo imezindua kituo mahiri cha usambazaji wa teknolojia za kilimo kilichopo Nzuguni, jijini Dodoma, kwa ajili ya Kanda ya Kati, kitakachotumika kushughulikia mahitaji ya wakulima, ikiwamo elimu kwa vitendo kwa wakulima katika eneo hilo wakati wote.

Lengo kubwa la kuwapo kituo hicho ni kuhakikisha kinatoa mchango katika kuboresha sekta ya kilimo nchini, kwa kuongeza, hivyo kutimiza agizo la Wizara ya Kilimo la kuongezwa tija na uzalishaji katika sekta kilimo.

Kanda ya Kati ni miongoni mwa maeneo yanayolimwa mazao ya biashara na chakula, zikiwamo zabibu, mtama, uwele, ulezi, mahindi, mihogo, kunde na mazao ya mafuta kama alizeti.

Hata hivyo, bado tija ya mazao hayo kwa sasa kwa wakulima walio wengi iko chini kutokana na matumizi hafifu ya teknolojia za kilimo bora na kwamba upande wa zao la mahindi tija yake ni tani moja na nusu kwa hekta, sawa na kilo 600 kwa ekari moja.




Washiriki wa Maonyesho ya Kitaifa ya Sayansi Teknolojia na Ubunifu, kuhusu namna teknolojia inavyotumika kuchochea mapinduzi ya kilimo nchini, katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma. **PICHA: TARI.**

**WAZIRI WA KILIMO**

Waziri wa Kilimo, Profesa Adolf Mkenda, akizindua kituo hicho cha usambazaji wa teknolojia, anasema kwamba changamoto kubwa ya wakulima, inaanzia kutotumia mbinu bora za kilimo bora.

Anataja upungfu mwingine kuwa ni kukosa stadi ya kutumia nafasi kati ya mmea mmoja na mwingine na utumiaji mbolea kwa usahihi, sambamba na viuatilifu.

Profesa Mkenda anayajumuisha yote, ni zao la kukosekana elimu bora ya huduma za kutumia ugani. Ana ufafanuzi: "Kwa hiyo, naamini kwamba kuanzishwa kwa kituo hiki kutaongeza ushirikiano kati ya wakulima, wagani na wadau wengine na kimeanzishwa muda mwafaka wakati wizara imeweka mkakati wa kuimarisha huduma za ugani nchini."

"Ni rai yangu kwa viongozi wa mikoa iliyo katika Kanda ya Kati watumie kituo hiki kuwajengea uwezo kwa vitendo maofisa ugani ili wasaidie kuwajengea uwezo wakulima katika maeneo yao ya kazi kusaidia kuongeza uzalishaji na tija, kuchangia kuwa na uhakika wa chakula, kipato, lishe bora na ukuaji wa uchumi kwa mtu mmoja mmoja, kaya na taifa kwa ujumla," anafafanua

Profesa Mkenda anaeleza imani yake kwamba, kituo hicho cha kusambaza teknolojia za kilimo, kitaendeleza malengo yake mahsusi ya mafunzo kutumia teknolojia za kilimo bora, mbegu za kisasa, kupanda kwa nafasi na matumizi sahihi ya mbolea na viuatilifu.

Pia, anawahakikishia Watanzania kwamba, kituo hicho kitatimiza jukumu lake la kutoa mafunzo kuhusu mbinu bora za kilimo katika mnyororo wa thamani, hata ikawa chachu ya kuwaunganisha wadau wa kilimo na masoko.

Katika eneo hilo, waziri anaahidi wizara itaanzisha kanzidata ya masoko ya mazao mbalimbali na kutoa huduma za ushauri wa kilimo biashara, ili kuwaongezea uwezo wakulima.

"Juhudi kubwa ikifanyika katika kutekeleza vizuri mipango hiyo, uzalishaji wa mazao utaongezeka, pia tija ya kilimo itapatikana, na

INAENDELEA UK.14

## KILELE SIKU YA WAZEE DUNIANI

# Tanzania imeshafikia mengi ya kujivunia?




Rais Samia Suluhu Hassan, alipozungumza na wazee wa mkoa Dar es Salaam kwa niaba ya wenzao kitaifa, mwezi Mei, mwaka huu, hotuba iliyotoa dira ya maslahi ya kada hiyo, nchini. Kulia ni walipokuwa wakimsikiliza katika ukumbi wa Mlimani City. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Joyce Bazira**

NI Jumamosi asubuhi, kwa mbali jua limeanza kuchomoza na kutengeneza nuru inayoipamba siku mpya. Katikati ya shamba la migomba, kuna nyumba kubwa ya udongo yenye bati kuukuu.

Hatua chache kutoka kwenye nyumba, kuna mti wa kivuli ambao chini yake kuna gogo kubwa. Kama afanyavyo siku zote asubuhi, Mzee Jackson Malebo, ameketi kwenye gogo, lakini tofauti na siku nyingine, leo amevalia nadhifu na uso wake umechangamka.

Majirani wanamshangaa, wanajiuliza maswali bila majibu, kila mtu anawaza lake. Kitu gani kipya kimetokea katika maisha ya Mzee Malebo? Fuatana na kazi ya mwandishi kupata maudhui ya makala hii, kupata uhondo wa siku 'leo' kwa kina.

Endelea:

### TUMAINI LA MABARAZA

NI siku ya 'leo' Oktoba Mosi ya kila mwaka, mataifa yote huadhimisha Siku ya Wazee Duniani. Tanzania inasherehekea, ikiwa na mengi ya kujivunia kutokana na mafanikio makubwa yaliyofikiwa katika kushughulikia kero za wenye kada hiyo ya umri.

Mzee Malebo, ni kielelezo cha wazee wengine nchini, ambao maisha yao yamebadilika, kutokana na mikakati iliyowekwa na wadau wanaoshirikiana na serikali. Wazee nchini sasa wana matumaini mapya na matarajio ya kuishi bila ya hofu, huku wakipata stahiki zao pasipo usumbufu

Kuanzishwa kwa mabaraza ya wazee takribani kote Tanzania Bara, ni miongoni mwa makubwa yaliyofanyika kuhakikisha kunakuwapo mfumo mzuri wa kuwafikia haraka wa kushughulikia changamoto zao kwa ufanisi.

Ni mabaraza yaliyoko katika ngazi mbalimbali, kuanzia ya kijiji, kata, wilaya na mkoa na mpango wa kuanzisha baraza moja la taifa lenye uwakilishi wa wazee kutoka kila mkoa uko mbioni.

Mkurugenzi wa Shirika la Kuhudumia Wazee Tanzania, HelpAge International, Daniel Smart, katika mahojiano maalum na mwandishi wa makala hii, anajinasibu kwa kauli:

"Wazee sasa wana majukwaa ya kuzungumza masuala yao kwa uhuru na bila hofu. Kupitia mabaraza hayo. Pia wanapata taarifa muhimu zinazowahusu na migogoro mingi inayowahusisha wazee, inapatiwa ufumbuzi kwa haraka na bila usumbufu wowote."

Smart anayasifu mabaraza hayo kwa kazi nzuri ya kupokea na kutafutua ufumbuzi wa masuala yanayowahusu wazee, akiweka sawa hoja yake kwa ufafanuzi: "Changamoto nyingi zinazowakabili wazee, zinamalizwa katika mabaraza huko huko maeneo wanayoishi, zile zenye sura ya kitaifa ndizo hufikishwa ngazi ya juu kupatiwa ufumbuzi."

Mnamo Juni 15 mwaka huu, Waziri wa Afya na Mandeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, amewaambia waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kupinga Ukatili Dhidi Wazee yanayoadhimishwa kila mwaka, kwamba serikali inawatambua wazee kwamba ni hazina ya taifa.

Dk. Gwajima anataja hazina hizo ni ujuzi na uzoefu walionao kiuchumi na kijamii, hivyo inahakikisha rasilimali hiyo inatumika vizuri kunufaisha umma yote.

Anasema, serikali inaendelea kuunda mabaraza yao nchini kote na hadi sasa yameshaundwa 14,883 kuanzia ngazi za vijiji na mitaa, kata, wilaya na mikoa nchini.

Joseph Mbasha, ni Meneja Miradi anayeshughulikia Ulinzi wa Uhusiano ya asasi ya HelpAge International, anayeorodhesha mafanikio yanayotokana na mabaraza hayo tangu kuanzishwa.

"Huko Kahama, kupitia baraza la wazee, watu walihamasishwa kuwakatia bima za afya wazee 300; mkoani Simiyu, baraza la wazee lilifanikiwa kuzuia matukio ya mauaji ya wazee yanachochewa na imani za kishirikina na huko Karagwe, mabaraza yamefanikiwa kuwaelimisha watu juu ya dhana nzima ya uzee naasa wana uelewa mpana na wanawajibika katika kuwahudumia" anasema.

Kwa mujibu wa Mbasha, mabaraza ya wazee yanasaidia kuimarisha amani na umoja katika jamii, huku yakichochea uwajibikaji wa mwananchi mmoja mmoja, katika kuwajali na kuwahudumia wazee mahali waliko.

Anasema, muundo wa mabaraza hayo ni mfano bora wa kuigwa na jamii, kwani unazingatia usawa wa kijinsia, kila moja lina wazee saba, wanaume kwa wanawake.

Mkurugenzi wa HelpAge International, Smart, hata hivyo anataja upungufu, kwamba bado mabaraza hayo yanaendeshwa chini ya Sera ya Wazee ya Mwaka 2003, kwa sababu hayajatungiwa sheria.

Anasisitiza bado kunakosekana sheria mahsusi, hali inayoikosesha msukumo stahiki, badala yake inaangukia hisani kwa wazee kutoka kwa kiongozi aliyeko madarakani.

### HAMASA YA MAADHIMISHO

Mafanikio mengine ambayo HelpAge na wadau wengine wanajivunia katika kuadhimisha siku yao, ni kufanikiwa kuwajengea Watanzania uelewa juu ya umuhimu wa siku hiyo.

"Wakati tulipoanza kuadhimisha siku ya wazee, watu wengi hawakuwa na uelewa juu ya siku hii muhimu na kutokana na hilo, tulilazimika kuibeba peke yetu, lakini hivi sasa wadau wana uelewa wa kutosha na serikali iko kwenye injini ikiratibu shughuli zitakazofanyika kwenye maadhimisho ya siku hiyo muhimu,"anasema Smart.

Anautaja ushirikiano mkubwa unaoonyeshwa na serikali, ni kioo cha mafanikio makubwa,

Meneja Miradi anayeshughulikia Ulinzi wa Uhusiano ya kitaasisi kutoka shirika la HelpAge International, Mbasha, anasema katika maadhimisho ya mwaka huu, wazee hawatakutana eneo moja na badala yake watabaki waliko, wakiwa na shughuli zao.

Mbasha anasema, serikali imeshatoa mwongozo wa vitakavofanyika na maofisa ustawi wa jamii wamepewa majukumu kusimamia shughuli hizo katika ngazi ya mikoa waliko.

Kwa mujibu wa ratiba ya maadhimisho hayo, kuanzia Septemba 27 hadi kilele chake leo, kila mkoa unatakiwa kuweka mabanda katika viwanja vya maadhimisho yanayoonyesha huduma mbalimbali kwa wazee.

Miongoni mwake ni; msaada wa kisaikolojia kwa wazee na familia zenye uhitaji; afya na chanjo ya UVIKO 19 na uelimishaji katika vyombo mbalimbali vya habari, kuhusu maadhimisho; na huduma kwa wazee.

Siku ya kilele ambayo ni 'leo', wazee kutoka halmashauri zote ndani ya mikoa, wananchi na wadau wengine wanashiriki pamoja kuadhimisha.

Mbasha anataja kaulimbiu ya mwaka huu ni "Matumizi Sahihi ya Kidigitali kwa Ustawi wa Rika Zote" ikimaanisha katika kipindi kilichoko cha athari za UVIKO 19, kuna taarifa nyingi za upotoshaji kuhusu ugonjwa huo, hivyo ni vema pakawapo utaratibu unaohakikisha wazee wanasaidiwa kupata taarifa muhimu, sahihi na zinazoendana na wakati.

### KIKAO CHAO NA WAZIRI

Dk. Edwin Mung'ong'o, Meneja wa Afya na Huduma kutoka HelpAge International, anafafanua kuhusu kikao hicho cha kila wiki mahsusi siku ya Jumamosi, anasema kinalenga kushirikisha wizara mbili; Afya na Mandeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Ofisi ya Rais (TAMISEMI), kupitia idara yake inayoshughulikia masuala ya wazee.

Katika mjumuiko huo, pia wamo HelpAge International na wawakilishi wa wazee kupitia Mtandao wa Wazee Tanzania, chini ya uenyekiti wa Waziri Dk. Gwajima.

"Uzuri wake ni kwamba wadau wote muhimu wanakuwa kwenye kikao kimoja na wakati changamoto zinazowakabili wazee zinapowasilishwa, Waziri huwauliza wahusika mmoja mmoja namna wanazitafutia ufumbuzi kero hizo," anaeleza Dk. Mung'ong'o.

Anasifu kuwa ni hali inayomfanya mtu awajibike kufanyia kazi kero zilizoelekezwa kwenye eneo lake, kwa sababu anawajibika katika kikao kinachofuata kukitolea ufafanuzi, hali inayojenga ukweli, mfumo wa haraka na uwajibikaji.

Vilevile, Dk. Mung'ong'o anasema ni namna inayorahisisha kubaini kero sugu zinazowakabili wazee kwa muda mrefu sasa na kuzipatia ufumbuzi.

### KUPUNGUZWA MAUAJI

Mafanikio anayoyataja ni maadhimisho ya mwaka huu, yatafanyika wakati mikasa ya mauaji kwa visingizio vya kuwapo imani za ushirikina inapungua kwa kundi hilo la jamii, HelpAge International inayarejea ni zao la kampeni za wadau mbalimbali ikiwamo serikali.

Siku ya Juni 15, mwaka huu, katika hotuba yake ya kufungua Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kupinga Ukatili dhidi ya Wazee, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mwanaidi Khamis, amesema jitihada kubwa zinazofanywa na serikali kwa kushirikiana na wadau, zimepunguza na kudhibiti ukatili na mauaji kwa wazee kwa kiasi kikubwa.

Naibu Waziri anarejea taarifa ya Jeshi la Polisi kwamba mauaji ya wazee yamepungua kiwango kikubwa, kutoka 577 mwaka 2014 hadi wazee 34 Desemba, mwaka jana.

Huku akikiri kipato duni kinachangia kuwaingiza katika ukatili na mauaji, Naibu Waziri anatoa mwelekeo mpya: "Serikali inalenga kuhakikisha wazee wanawezeshwa katika kubuni na kuendesha shughuli za ujasiriamali kupitia vikundi vidogo vidogo kwenye jamii, ili kuwawezesha kuinua kipato na kumudu mahitaji yao ya msingi."

### ANDIKO LAO SERIKALI

Mkurugenzi wa HelpAge International, Daniel Smart, anasema yamebaki maeneo kadhaa yanayoendeleza kero kwa wazee nchini hivyo kuna andiko linaloainisha changamoto zao, lililokwishawasilishwa kwa waziri mwenye, Dk. Gwajima, katika kikao kazi mwezi ulioisha jana.

Kwa mujibu wa Smart, maudhui yake yameainisha maeneo makuu yanayoleta kero kwa wazee, mosi ni katika hitaji la kupatiwa huduma bora ya afya, ikienda eneo maalum la upatikanaji dawa.

Inaelezwa, licha ya serikali kuelekeza haja ya huduma kwa wazee zitolewe bila malipo na wapewe vitambulisho, bado kuna ugumu wa vitambulisho vinavyotumika katika mikoa vinakotolewa pekee na anapopatwa na dharura nje ya mkoa wake, hapati huduma inavyostahili.

Kadhalika, kuna malalamiko ya dawa za magonjwa yanayowahusu wazee wengi, hasa yasiyo ya kuambukiza hazipatikani kila mara kwenye vituo vya utoaji huduma

"Tunaomba vitolewe vitambulisho vya matibabu kwa wazee vinavyowaruhusu kupata matibabu katika ngazi na vituo vyote.

"Pia, tunashauri bodi na kamati za afya katika vituo vya kutoa huduma ziwe na uwakilishi wa wazee, ili wafuatilie ununuzi na matumizi ya dawa za wazee," inafafanua sehemu ya andiko hilo la wazee.

Lingine ni kwamba, wazee hao wanalalamika kutotungiwa sheria, hali inayowasababisha wakose mambo mengi yenye msukumo kisheria, hivyo wanahudumiwa zaidi katika mtazamo wa hisani.

Pia, kuna ombi la msamaha wa kodi ya majengo yanayomilikiwa na wazee, kwani bado ni changamoto kwao. Kwa mujibu wa andiko hilo, serikali ilitoa msamaha wa kodi ya majengo kwa nyumba zinazomilikiwa na wazee za kuishi pekee na si biashara na kila mwaka mzee anatakiwa kuandika barua kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuomba msamaha wa kodi ya majengo.

"Tunashauri ofisi za TRA kote nchini zielekezwe kuzingatia maelekezo ya msamaha huu, elimu itolewe kuhusu msamaha huo, pia mzee akishatambuliwa asamehewe moja kwa moja bila kutakiwa kuandika barua kila mwaka.

"Pia, tunashauri uangaliwe utaratibu wa kusamehe kodi ya ardhi kwa nyumba zinazomilikiwa na wazee," linafafanua andiko hilo.

Eneo lingine linahusu kipato duni cha jamii ya wazee, ni kero wanayoishauri serikali kuangalia wale wenye umri zaidi ya miaka 65 wapatiwe pensheni jamii kama inavyofanyika Tanzania Visiwani.

Andiko linagusa haja ya uwakilishi wa wazee katika vyombo vya kuamua, ikishauriwa utolewe mwongozo kwa halmashauri zote nchini kuwaruhusu wawakilishi wazee katika vikao vya maendeleo (WDC), kuwawezesha wazee wapate haki ya kupiga kura na kuamua yanayohusu hatima ya maendeleo yao.

Kwingine ni hitaji la uwakilishi wao bungeni nchini, waweze kuwasilisha hoja na kero zao, ikayowafanya wawe hai katika mipango na programu za maendeleo ya nchi.

Andiko linashauri wizara inayohusika na afya, kusimamia utaratibu unaowezesha Azimio la Afrika kuhusu Haki za Wazee la Januari 31, mwaka 2016 kupitia viongozi wa nchi wanachama ikiwamo Tanzania, litiwe sahihi na hatua zote zinazotakiwa katika kuliridhia ianze kutekelezwa.

Kwa mujibu wa hoja hiyo, kuridhiwa azimio kutaiweka nchi katika ramani nzuri ya kujaliwa maslahi ya wazee kitaifa.

Takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012, inataja idadi ya wazee nchini wako 2,507,568, kati yao 1,200,210 ni wanaume na 1,307,358 wanawake, wakiwa sawa na asilimia 5.6 ya Watanzania wote kwa wakati huo,

### DHAMIRA ILIYOKO MBELE?

Kuna baadhi ya mambo kwa mujibu wa HelpAge, yanayoonyesha dhamira ya serikali kutoa kipaumbele kwa magumu yanayowakabili wazee nchini, ikitaja kitendo cha Rais Samia Suluhu Hassan, alipotafuta faragha na kuzungumza na wazee wa Mkoa wa Dar es Salaam, kwa niaba ya wenzao nchi nzima, mara baada ya kuingia madarakani.

Katika mazungumzo hayo ya Mei 7, mwaka huu, Rais Samia, amewahakikishia ushirikiano katika masuala yote yanayowahusu na amekaririwa akitaja maeneo kama maboresho ya kisera, pia afya ambalo limo katika ilani ya kisiasa, akikiri inasukuma zaidi kuwawajibikia

"Tunatambua dunia iko kwenye janga la korona na wanaoathirika zaidi ni wazee, hivyo nataka nitoe taarifa kwa wazee, kamati ambayo nimeiunda itatoa taarifa, " amekaririwa Rais kwenye kauli yake.

# TARI yafungua kituo Dodoma kuweka sawa uzalishaji shambani Kanda Kati

INAENDELEA UK.11

jambo muhimu na la kuzingatia ni kufanya shughuli za kituo hiki cha TARI kuwa endelevu kwa kuweka mpango mkakati unaolenga kutoa mafunzo," anasema.

Waziri Mkenda anazitaka halmashauri nchini zote kutoa fedha za kutosha kwa ajili ya kuendesha shughuli za usambazaji wa teknolojia bora za kilimo na kuimarisha huduma za ugani nchini.

Pia, anasema Tanzania imekwama kuuza baadhi ya mazao nje ya nchi, kutokana na kukosa tija kwa mazao hayo na hata pale walipopata soko la kufanya hivyo hawakufanikiwa kuyaingiza sokoni.

"Kwa mfano zao la muhogo, tumeshindwa kuuza nje ya nchi kwa sababu halina tija, uzalishaji wake bado siyo wa kuridhisha. Siyo hilo tu, karibu mazao yote bado kuna tatizo kubwa ambalo bado tuna kazi kubwa ya kufanya kuondoka hapa tulipo," anasema Profesa Mkenda.

Anasema kazi kubwa inayotakiwa kufanyika sasa ni kuinua sekta hiyo ya kilimo, ili kuongeza nguvu katika kutumia tafiti kwenye sekta kuzalisha mbegu bora na kuimarisha shughuli za ugani.

Waziri anaeleza kwamba TARI kwa sasa imefanya kazi kubwa ya utafiti kwa ajili ya kuinua sekta hiyo na kwamba, ni vema nao wakulima wakatumia utafiti huo kwenye shughuli zao ili kuboresha sekta hiyo ya kilimo ilete tija.

"Tunaamini kwamba wakulima wakitumia tafiti hizi za TARI kwenye kilimo, watakuwa wanazalisha mazao mengi, bei itakuwa chini lakini wakulima bado watapata kipato.

"Hakuna atakayeumia, si mlaji wala mkulima, lakini kwa sasa kwa mfano tunalia mafuta ya alizeti au chakula fulani kimepanda, hii ni kwa sababu mazao yetu hayana tija," anasema Profesa Mkenda.

**BOSI MKUU TARI**

Mkurugenzi Mkuu wa TARI Tanzania Dk.Geoffrey Mkamilo, anasema taasisi hiyo imejipanga kuhakikisha mchango wake unasaidia kwa kiwango kikubwa, kuinua sekta hiyo ya kilimo nchini.

Anasema, hiyo si kwa eneo la kuzalisha mazao ya kutosha kwa ajili ya chakula, lakini kubwa zaidi ni kuona wakulima wanazalisha mazao biashara kukidhi mahitaji ya ndani na nje ya nchi.

"Lengo ni kuona kilimo kinanyanyuka zaidi, tunataka wakulima nao waone umuhimu wa kutumia tafiti zetu kwenye shughuli zao za kilimo kwa sababu hili ndilo suluhisho pekee la kukifanya kiwe bora na kuzalisha kwa wingi," anasema Dk.Mkamilo.

"Sisi TARI tumefanya tafiti nyingi ambazo wakulima wakizitumia watafika mbali sana na hakuna kiwanda ambacho kitakosa malighafi, vyote vitapata ya kutosha, kwa hiyo tunawaomba waache kulima kwa mazoea," anasema

Anafafanua, kwa sasa uzalishaji unashuka kutokana na wengi kushindwa kufuata kanuni za kilimo bora, ikiwamo kutumia mbegu bora na zana bora.

"Ndio maana tumeamua kuanzisha hivi vituo hivi vya usambazaji teknolojia za kilimo za TARI na kwa nchi nzima mpaka sasa vimefikia nane. Lengo ni kuhakikisha kwamba, wakulima wanatumia teknolojia kuwa na kilimo cha kisasa ambacho kitaleta mabadiliko," anaeleza Dk. Mkamilo.

"Kwa hiyo tunaamini kwamba, wakitumia teknolojia hizo na kufuata mbinu zote bora za kilimo pamoja na tafiti zetu, kilimo kitakuwa sana. Vituo hivi tunavyoanzisha vitatumika kutoa huduma mwaka mzima za elimu kwa wakulima, maofisa ugani na huduma mbalimbali, anahitimisha."




Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk.Geoffrey Mkamilo. **PICHA: TARI.**

## TAFAKURI YA MLALAHOI

# Uviko-19, Wamachinga wasitugombanishe






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
jkulangwa@yahoo.com

WATANZANIA hivi sasa wanakabiliwa na mambo makubwa mawili ambayo si ya kudumu, lakini yanawaumiza vichwa; Uviko-19 na Wamachinga.

Suala la Uviko-19 linasumbua kiasi kwamba baadhi ya watu wanaona kama halipo, ingawa linaendelea kuua. Lakini, watu wameshikwa na ganzi, wapo wanaoliona tatizo na wengine wanaona kawaida.

Wanaoliona ni tatizo ndio hao wanakwenda kuchanja kwa hiari kwa mujibu wa msimamo wa serikali, lakini wanaona la kawaida, hata kuvaa barakoa wanaona ni kero kwao, kana kwamba maisha yao wameyaazima.

Ukiambiwa kuwa dozi zaidi ya milioni moja zilizotolewa na kampuni ya Johnson & Johnson ya Marekani kwa Tanzania, mpaka sasa iliyotumika haifiki hata nusu yake, ni jambo la kushangaza.

Licha ya Rais Samia Suluhu Hassan kujitokeza hadharani, akiwa na ufafanuzi wa kina binafsi mpaka anafukia uamuzi kuchanja, bado watu wanaona si tija, inashangaza sana!

Haiwezekani kwamba kauli ya kuchanja ni hiyari, basi ndiyo ihalalishe watu kuambukizana, kwa kuwa hawana chanjo. Kuna jambo linapaswa lifanyike kuepuka maangamizi ya Uviko-19.

Si kwamba watu nchini hawafi kwa ugonjwa hilo, wanakufa. Lakini nini kifanyike, kama chanjo ni ya hiari? Watu walazimishwe, hapana! Waachwe waangamize wenzao kwa uzembe tu, hapana!

Wanasimama viongozi wa dini kulalamikia viongozi wa serikali ambao wanahimiza chanjo, lakini wao hawachanji, inakuwaje? Mathalan yupo kiongozi wa dini ambaye hakutaka kumung'unya maneno, ana yake kwa kina.

Anashangaa katika dozi lakini kasoro zilizotengwa kwa jiji aliko, mpaka sasa hazijamalizika. Maana yake watu hawachanji. Anatoa mfano wa viongozi na hata watumishi wa serikali walioko jijini humo, kwamba wangechanja dozi hizo zingeshaisha.

Nini kinazuia watu kuchanja? Ni dhana iliyowahi kujengeka, chanjo haiaminiki? Je, ni kauli za baadhi ya viongozi kuwa chanjo zina madhara?

Je, yawezekana dhana kupitia imani pekee, Uviko-19 itaondoka yenyewe? Au ni utaratibu wa mchanjwa kabla ya kuchanjwa kusaini hati ya kiapo kuwa athari hasi ikitokea asilalamike?

Yote hayo yanaweza kuwa yamechangia mpaka kufikia hali tuliyo nayo hivi sasa, licha ya juhudi za Rais kuhimiza, wataalamu kuhimiza, serikali kuanzisha chanjo kufuata watu waliko na hata viongozi wa soka nchini kuweka utaratibu maalumu wa watazamaji soka kuchanja kabla ya kuingia viwanjani.

Pia kuna cha kujiuliza, yote haya yakifanyika kikamilifu, watu wakachanja tutaepuka Uviko-19 licha ya mikusanyiko hii inayoendelea karibu kila mahali kwa matamasha? Tutafakari.

Hili la Wamachinga la kuwahamishia maeneo maalumu halijaanza leo. Limekuwa likiimbwa karibu miaka yote, lakini bila hatua kuchukuliwa, ama kwa makusudi au kwa sababu maalumu za kisiasa.

Wamachinga hawakuanza leo, lakini waliibuka kama uyoga wakipita mitaani kuchuuza bidhaa zao mikononi. Walipoongezeka na kuonekana wapiga kura wazuri, wakaachwa na kusimika vibanda taratibu mitaani.

Polepole wakafurika na kuziba hata maduka halali yanayolipa kodi serikalini, kwa sababu tu mmachinga alikuwa kahalalishwa. Wenye maduka nao wakaona isiwe tabu, wakafungua maduka, lakini bidhaa wakagawia wamachinga hao hao kuuza bila kodi.

Leo Wamachinga wanaonekana kikwazo kwa wafanyabiashara, pia kwa serikali inayotegemea kodi. Serikali imeamua sasa kuwahamishia kunakohusika, maeneo maalumu ambako wataendesha biashara zao bila ya kubugudhi wafanyabiashara wenye maduka.

Dar es Salaam chini ya mkuu wake, Amos Makala, imeshaanza kutekeleza hilo kwa kuwahamisha, tena ikiwahusisha wamachinga wenyewe, lakini tayari kelele zimeanzaza kutaka kuonyesha kuwa wanaonewa.

Mmoja wa wanasiasa katika malalamiko yake kupitia fursa yake, anasikika hata akirushia kauli kali na fedheha kwa viongozi akiwatamkia wanaowabugudhi wamachinga na kuwaonea. Ni kauli yenye ukakasi.

Suala la Wamachinga lisitugombanishe Watanzania, bali litekelezwe kwa umakini, weledi na staha kubwa, hatimaye wawe na mahali maalumu pa bishara na si kujazana katikati ya miji kuzuia mapito na maduka. Haivumiliki kokote duniani.

Waondolewe, wapewe maeneo maalumu leo na isisubiriwe wakati joto la siasa liko juu hata kila mtu anafanya atakalo anaona ana uhuru, ili mradi dhana yake ni sawa na kwa maslahi yake, ili mradi kinachoangaliwa maslahi yake kisiasa. Alamsiki!



# Serikali kujenga vyuo vya watu wenye ulemavu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya watu wenye ulemavu, Ummy Nderiananga, amesema serikali imedhamiria kujenga na kukarabati vyuo vya watu hao ili kuwasaidia kupata ujuzi na kujikomboa kiuchumi.

Nderiananga aliyasema hayo jijini hapa baada ya kupokea msaada wa vifaa visaidizi kwa ajili ya wenye ulemavu vyenye thamani ya Sh. milioni 13.9 kutoka kwa Taasisi ya kutoa huduma ndogo za kifedha (ASA Microfinance Company Limited).

Alisema dhamira ya serikali ni kuhakikisha kila Mtanzania anapata haki yake bila vikwazo.

"Ipo mikakati madhubuti ya kuhakikisha masuala ya wenye ulemavu yanapewa kipaumbele ikiwamo uboreshwaji wa vyuo kikiwamo Chuo cha Mwanza ambacho kinatarajiwa kukamilika kuanzia mwezi Januari mwakani."

"Kwasasa wizara inaratibu kwa kasi ujenzi wa vyuo vya watu wenye ulemavu na ufufuaji wa vile ambavyo vipo. Tunaendelea kufanya hivyo katika Chuo cha Yombo Dar es Salaam, tumezindua chuo kingine Tabora ambacho kilikuwa kimefungwa kwa miaka 10 na kumalizia ujenzi wa chuo cha kisasa Mkoa wa Tanga," alisema.

Alisema kuwa serikali imeweka mkazo kuwasaidia watu wenye ulemavu kwa kuendelea kutoa fedha ya elimu bila malipo na watu wenye ulemavu nao wananufaika.

"Serikali kupitia bohari kuu ya dawa inaendelea kuagiza mafuta ili kuwakinga dhidi ya saratani ya Ngozi kwa watu wenye ualbino sambamba na kuzitaka Halmashauri kuendelea kutenga fedha za mapato ya ndani kupitia asilimia 10 inayotolewa na kila halmashauri kwa wanawake, vijana na wenye ulemavu kwa sababu hii inawasaidia kupambana na umasikini,"alieleza.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa ASA Microfinance Limited, Muhammad Shah Newaj, alisema kwamba wametoa msaada huo kama sehemu ya kutambua mchango wa watu wenye ulemavu katika maendeleo kuanzia ngazi ya familia hadi taifa.

Naye, Ofisa Sheria kutoka ASA Microfinance Limited, Zephania Paul, alisema taasisi hiyo ipo katika mikoa nane ya Tanzania Bara na Zanzibar na hadi sasa wamewafikia wanawake 1,600 na kutoa ajira.

# TAMISEMI kuja na mwongozo wa uendeshaji halmashauri

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), ipo kwenye mchakato wa kuangalia gharama za uendeshaji wa halmashauri zote nchini ili kuja na mwongozo wa matumizi ya fedha hizo.

Waziri wa Ofisi hiyo, Ummy Mwalimu, alitoa kauli hiyo alipokuwa akifunga mkutano wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa (ALAT), uliofanyika jijini hapa.

Waziri Ummy alisema hatua hiyo imetokana na ombi la Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Murshid Ngeze, ambaye aliiomba serikali kuangalia mgawanyo wa fedha za mapato ya ndani kwa uendeshaji wa halmashauri na zile zinazopelekwa kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Alisema kutokana na mgawanyo huo imekuwa vigumu kwa halmashauri kujiendesha hasa zenye mapato madogo.

Alisema maelekezo ya kupeleka asilimia 40 kwa halmashauri zenye mapato kidogo na asilimia 60 kwa zile zinazokusanya zaidi ya Sh. bilioni tano utaendelea kutekelezwa na kusimamiwa.

"Kamati inayoongozwa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-TAMISEMI inapitia na kuangalia tena gharama za uendeshaji katika halmashauri zote zenye mapato makubwa na zile zenye mapato kidogo ili baadaye kuja na mwongozo wa namna bora ya matumizi ya fedha za uendeshaji."

"Tumeangalia gharama za posho za kamati za kudumu za Halmashauri, vikao na ufuatiliaji wa miradi, posho za mwezi kwa zile Halmashauri zinazolipa, uendeshaji wa ofisi za kata na vijiji, wenyeviti mitaa, posho za wenyeviti wa halmashauri, kata pamoja na matumizi mengineyo," alisema.

Aidha, alisema posho za wakuu wa idara na vitengo, watendaji wa kati, watumishi wa mikatataba, vikao vya kisheria na mabaraza.

"Tunakuja na mwongozo utakaobainisha kiasi cha fedha za kuendesha halmashauri zenye mapato ya chini sambamba na zile zenye mapato makubwa, maana unaweza kuangalia ukakuta halmashauri inakusanya Sh. bilioni tano gharama za uendeshaji ni Sh. bilioni mbili, lakini kuna halmashauri inayokusanya Sh. milioni 600 na gharama ya uendeshaji ni Sh. milioni 360 tu."

"Unajiuliza hawa wanawezaje kuendesha halmashauri kwa Sh. milioni 300 ilhali wengine wanaendesha kwa Sh. bilioni mbili, hivyo lazima tutoe mwongozo hata kama una mapato makubwa tufahamu hizo fedha zinatumikaje," alisisitiza Waziri Ummy.

Alisema fedha za mapato zinakwenda kuleta maendeleo, shida za wananchi zinatatuliwa, lakini pia kuhakikisha maslahi yanazingatiwa na wakati huo huo fedha zinarudi kwa wananchi kwa njia ya maendeleo.

Aliwataka mameya, wenyeviti na wakurugenzi kuhakikisha wanakusanya mapato ipasavyo na kusisitiza kuwa endapo halmashauri haitafanya vizuri katika eneo la ukusanyaji wa mapato Mkurugenzi atakuwa hatoshi katika hiyo nafasi.



Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa (katikati), akifafanua jambo kwa makandarasi wa kampuni ya Inter-Consult Ltd, inayojenga barabara ya mzunguko ya urefu wa kilometa 112.3, jijini Dodoma, wakati alipokuwa akikagua maendeleo ya ujenzi wa mradi huo. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Barabara ya mzunguko kuanza ujenzi wiki hii

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema mradi wa ujenzi wa barabara ya mzunguko jijini Dodoma utaanza wiki hii katika kipande cha Nala, Veyula, Mtumba na Ihumwa cha Kilometa 52.3 sambamba na kipande cha Ihumwa, Matumbulu hadi Nala chenye urefu wa kilometa 60.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa alibainisha hayo baada ya kukagua vipande vyote viwili vyenye jumla ya kilometa 112.3.

Prof. Makame alisema hakuna haja kuchelewa kwenye utekelezaji wa mradi huo kwa kuwa makandarasi wapo tayari na wameshafanya maandalizi ya awali kuanza kazi rasmi.

Alisema pia asilimia kubwa ya wananchi tayari wameshalipwa fidia na kwa wale ambao bado mchakato unaendelea.

"Mradi huu sasa utaanza rasmi tumeona vifaa vingi vimeshaletwa na wananchi wengi wameshalipwa fidia na hao wengine waliobaki mchakato unaendelea," alisema Prof. Mbarawa.

Prof. Mbarawa aliwasisitiza makandarasi wa vipande vyote viwili kuanza kazi haraka na kujenga kwa viwango vinavyostahili ndani ya miezi 33 badala ya 36 kama ilivyo kwenye mkataba ili kuruhusu wananchi kunufaika mapema na mradi huo.

"Makandarasi jipangeni vizuri ili kazi hii ifanyike ndani ya miezi 33 na kwa viwango vinavyostaili, sio barabara zinajengwa baada ya mwaka au miaka miwili zinaharibika," alisema.

Waziri Mbarawa alitoa wito kwa wananchi watakaopata ajira kwenye mradi huo kuhakikisha wanafanya kazi kwa kujituma na uaminifu ili kujenga imani kwa makandarasi hao na kutoa ajira nyingi kwa wazawa.

Kwa upande wake, Msimamizi wa Mradi, Mhandisi Salikiheri Munisi, alisema tayari wameshaleta vifaa kwenye eneo la mradi na kinachosubiriwa sasa ni kukamilisha baadhi ya mambo machache ili kuanza ujenzi rasmi.

Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Mkoa wa Dodoma, Mhandisi Salome Kabunda, alisema kuwa mradi huo umepita kata zisizopungua 10 na baadhi ya wananchi wameshalipwa fidia.

Alifafanua kuwa hadi sasa kiasi cha Sh. bilioni 12.76 zimelipwa kwa jumla ya wananchi 2,338 kati ya 2,800, na kusisitiza kuwa serikali inaendelea na mchakato wa kuwalipa wale waliobakia.





# Halmashauri zaagizwa maziwa shuleni

**NA Grace Mwakalinga,** MBEYA

KATIKA kukabiliana na tatizo la udumavu mkoani Mbeya, Mkuu wa Mkoa huo, Juma Homera, amewaagiza wakurugenzi wote wa Halmashauri katika mwaka wa fedha 2021/2022 kutenga fedha kwa ajili ununuzi wa maziwa shuleni.

Homera alitoa kauli hiyo jana akifunga kilele cha wiki ya unywaji maziwa nchini ambapo kitaifa yaliadhimishwa mkoani Mbeya na kushirikisha wadau mbalimbali katika tasnia ya maziwa pamoja na wanafunzi wa shule za Msingi.

Alisema tasnia ya maziwa ni muhimu kwa maendeleo ya ukuaji wa watoto, kwani huchangia kuimarisha afya ya akili na kusaidia watoto kuwa na uelewa mzuri.

Kutokana na hali hiyo, aliziagiza halmashauri zote kutenga bajeti kwa mwaka wa fedha ujao ili watoto waanze kunywa maziwa, lengo likiwa ni kujenga afya zao na kuongeza ufaulu.

"Tunataka taifa lenye watu wenye akili timamu na unywaji wa maziwa unachangia kwa kiasi, udumavu wa akili na mawazo shuleni utaondolewa kwa kunywa maziwa wakurugenzi angalieni namna ya kupata fedha jambo hili nimelibariki hivyo ni utekelezaji tu," alisema Homera.

Alisema hali ya udumavu mkoani Mbeya kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2018 ilikuwa ni zaidi ya asilimia 30 na kwamba kwa mujibu wa utafiti usio rasmi ambao umefanywa na wataalamu Mbeya imejitahidi kukabiliana na tatizo hilo ambapo inakadiriwa kuwa na asimilia 20 kwa sasa.

Aliwataka wadau kuanzisha viwanda vya maziwa mkoani Mbeya kwa kuwa ni miongoni mwa mikoa saba nchini ambayo inaangoza kwa kuwa na wafugaji wengi wa ng'ombe ambapo inakadiriwa kuwa na ng'ombe zaidi ya milioni moja.

Alisema tasnia ya maziwa mbali na kuwa mlo kamili pia inasaidia kuongeza pato la taifa na kusaidia wananchi kujikwamua kiuchumi kwa sababu baadhi ya wafugaji wanauza bidhaa hiyo na kujiingizia kipato.

Mwakilishi wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo, Steven Michael, alisema kuwa licha ya Tanzania kuwa ya pili kwa ufugaji wa Ng'ombe barani Afrika bado unywaji wa maziwa upo chini.

Alisema Shirika la Afya Duniani (WHO) limependekeza kuwa angalau mtu mmoja anywe lita 200 za maziwa kwa mwaka, lakini Tanzania unywaji wa maziwa ni chini ya lita 50 na kueleza kuwa upo umuhimu wa kusisitiza ili kufikia lengo hilo.

Aliongeza kuwa Wizara hiyo, kupitia Bodi ya Maziwa Tanzania inakusudia kuanzisha program ya mashamba ya kibiashara ya ufugaji wa ng'ombe wa maziwa ambapo mpango huo utakwenda sambamba na ujenzi wa vituo vya ukusanyaji maziwa.

Katika kilele cha maadhimisho ya wiki ya unywaji maziwa nchini ambayo yaliadhimishwa mkoani Mbeya, zaidi ya wanafunzi 200 wa shule za Msingi walipewa maziwa sambamba na wazazi pamoja na walimu walioshiriki maadhimisho hayo lengo likiwa ni kuhamasisha unywaji wa maziwa nyumbani na shuleni.




Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (mwenye koti jeusi), akinywa maziwa wakati akifunga kilele cha maadhimisho ya wiki ya maziwa nchini ambapo kitaifa yalifanyika mkoani Mbeya juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Vijana wapewa siri kufanikiwa kiuchumi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

VIJANA mkoani Mbeya wameshauriwa kuchangamkia fursa mbalimbali zinazojitokeza kupitia mashirika na taasisi ili kujikwamua kiuchumi badala ya kujiingiza kwenye makundi yasiofaa na kuharibu ndoto za maisha yao.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Mkurugenzi wa Shule za Paradise Mission Pre&Primary School za mikoa ya Mbeya na Dar es Salaam, Ndele Mwaselela, alipozungumza na Nipashe.

Alisema vijana ili vijana waweze kutimiza malengo yao, lazima kuheshimu ndoto za maisha yao badala ya kushiwishika na wenzao na kujiingiza kwenye makundi yasiyofaa.

"Mimi ni miongoni mwa vijana wa mfano mkoani Mbeya, niliaza kufanya shughuli ndogo kabisa mama yangu akiwa ni mjasiriamali wa kuuza chakula nilikuwa na ndoto zangu nilihakikisha kwa namna yoyote natimiza nilijiepusha na makundi maovu na nilifanya kazi kwa bidii hadi sasa namiliki shule na miradi mingine," alisema Mwaselela.

Aliwashauri vijana kuchangamkia fedha za asilimia 10 za mikopo inayotolewa na Halmashauri kwa kuhakikisha wanajiunga kwenye vikundi ili waweze kukopesheka na kuanzisha shughuli za kujikwamua na umasikini.

Kwa upande wake, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mbeya, Suma Fyandomo, alisema katika kuhakikisha wananchi wa Mkoa huo wanafanya shughuli zao wakiwa na afya alitoa Sh. milioni 15 kwa ajili ya kuwakatia bima wananchi 500.

Alieleza sababu ya kufanya hivyo ni kuhakikisha wananchi wanapata matibabu bila kikwazo chochote ili kuendelea na shughuli zao za uzalishaji mali bila tatizo.

# Wadau waona fursa ya mkataba wa eneo la biashara

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WADAU, wawekezaji na wajasiriamali kutoka Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, wameipongeza Serikali kuridhia mkataba wa eneo huru la biashara kwa nchi za Afrika.

Wamesema hatua hiyo ni fursa na itachangia ukuaji wa uchumi kwa Taifa na mtu mmoja mmoja.

Akizungumza jana katika Kongamano la Wawekezaji na Wafanyabiashara wa Mikoa ya Mbeya, Ruvuma, Rukwa, Iringa, Njombe na Katavi, Msimamizi wa Sera kutoka Taasisi ya Sekta binafsi Tanzania (TPSF), Faith Gugu alisema kwa sasa Tanzania inahesabika kuwa miongoni mwa eneo huru la biashara Afrika.

Kutokana na umuhimu huo mwamvuli wa sekta binafsi Tanzania, waliendesha kongamano hilo kwa lengo la kujadili vikwazo na fursa zinazopatikana nchini na namna bora ya kunufaika kupitia eneo huru la biashara ukanda wa bara la Afrika.

"Tumekutana kujadili fursa mbalimbali tutakozipata baada ya kufunguliwa kwa eneo huru la biashara Afrika ni muhimu kupitia bidhaa zetu kuwa wabunifu ili kuwa washindani wazuri na wengine sambamba na kujadili vikwazo tunavyopitia ili tujadili na kutatua kwa pamoja kabla ya kuingia kwenye ushindani huo," alisema Gugu.

Akimuwakisha Mkuu wa Mkoa wa Mbeya Juma Homera, katika Tawala Msaidizi (Uchumi na Uzalishaji) , Mkoa wa Mbeya, Said Madito, alisema ni wakati sasa Wizara ya Viwanda na biashara kuandaa mkakati maalum kwa kuwawezesha wajasiriamali namna bora ya kuwa washindani katika eneo hilo.

Alisema ushirikishwaji wa wafanyabiashara na wawekezaji kujadili namna bora ya kutumia fursa hiyo utasaidia kuongeza thamani ya uzalishaji wa bidhaa na kufungua soko la mazao mbalimbali kama vile mahindi, maharage ambayo kwa sasa nchini soko lake sio la uhakika.

Miongoni wa washiriki wa kongamano hilo akiwamo, Mkurugenzi wa Masoko kutoka kampuni ya Mbasiro Food Industies Limited, iliyopo mjini Sumbawanga katika Mkoa wa Rukwa, Sylivery Buyaga, alisema kampuni yake inajishughulika na uchakataji wa mazao ya nafaka, hivyo kuwa sehemu ya kusaidia wakulima kuwakwamua na umasikini.

Alisema kongamano hilo limeleta matumaini kwao, kwani watashirikiana na serikali kutafuta mazao ndani na nje ya nchi ili kusaidia wakulima kuuza mazao yao nje ya Tanzania.

# Wimbi la talaka labebesha mzigo wazee kulea wajukuu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIMBI kubwa la talaka kwa wanandoa Zanzibar limesababisha wazee kubebeshwa mzigo mkubwa wa kulea wajukuu kutokana na baba na mama kuachana.

Hayo yalielezwa jana mjini hapa na Selwa Ali Sheha, Ofisa kutoka Idara ya Ustawi wa Jamii wakati akizungumza na waandishi wa habari katika warsha maalum kuhusu siku ya Wazee duniani ambayo huadhimishwa kila mwaka Oktoba 5.

Alisema wazee wengi wanakabiliwa na hali ya umasikini na kipato kidogo hivyo kubebeshwa jukumu la kulea wajukuu ni kuwaongezea mzigo wakati wazee wanahitaji matunzo na msaada kutoka kwa jamii, kutuzwa na kuthaminiwa.

Alisema karibu watu 50,000 wenye umri wa zaidi ya miaka 60 wanaongoza kaya (asilimia 16 ya kaya zote) za Zanzibar na mara nyingi hutunza pia wajukuu zao wakiwamo yatima.

"Theluthi mbili ya wazee wa miaka 60 na kuendelea bado wanafanyakazi ambapo asilimia 80 wanaume na 50 wanawake, lakini asilimia 60 hawapati mapato yoyote ya kujikimu, wengi wao wako katika sekta ya kilimo isiyokuwa na tija kubwa, wazee wengine hawapati msaada kutoka mahali popote, pia wanakabiliwa na matatizo ya afya na kutojiweza," alisema.

Naye Dk. Salum Ramadhan Muhamed, kutoka Idara ya Ustawi wa Jamii, alisema sera ya hifadhi ya jamii inaangalia kwa upana mahitaji ya wazee pamoja na makundi mengine katika kuzifikia huduma zote za msingi, ikiwamo suala la pensheni jamii, kupatiwa vitambulisho, huduma za afya na usafiri.

Alisema mazingira ya utoaji wa huduma kwa taasisi za kifedha bado haziko rafiki kwa wazee, taasisi nyingi za kifedha bado haziwaangalii wazee kama ni wateja muhimu, na hasa katika mikopo na benki chache hutoa mikopo kwa wastaafu pekee.

Alisema wazee wanakabiliwa na changamoto nyingi ikiwamo uchovu wa miili kutokana na wengi wao kufanya kazi ngumu wakati wa ujana wao, maradhi mbalimbali na hasa yasiyo ya kuambukiza na yale yakuambukiza wao huathirika zaidi, kama UVIKO-19.

Alisema pia wazee wanakabiliwa na changamoto ya lishe duni inayodhoofisha afya na miili yao, kudhalilishwa na jamii iliyowazunguka na kusingiziwa uchawi, kutengwa na jamaa na jamii zao na kukosa misaada stahiki katika maeneo mbalimbali.

Aliwataka waandishi wa habari kuripoti matatizo yanayowakumba wazee na kuyafanya yaeleweke na watunga sera na kufanya utafiti mbalimbali ya mambo yanayowahusu wazee.




Ofisa Mwandamizi Idara ya Ustawi wa Jamii na Wazee, Dk. Salum Rashid Mahamed (kulia), akifafanua jambo katika mkutano wa kuongeza uelewa kwa waandishi wa habari, jijini zanzibar jana, kuhusu masuala yanayowahusu wazee na wajibu wao katika kusukuma utekelezaji wake. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Ataka mazingira bora upatikanaji elimu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

DIWANI wa Wadi ya Dimani, Khamis Omar Khamis, amesema mazingira bora ya upatikanaji wa elimu kwa wanafunzi yatawawezesha kufanya vizuri na kufaulu mitihani yao.

Hayo aliyaeleza juzi wakati akikabidhi vifaa vya masomo na vyakula kwa wanafunzi wa Shule tano zilizomo katika jimbo la Dimani Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Alisema wanafunzi siku zote wanahitaji kuwa katika hali nzuri ya ufundishaji na mazingira mazuri ambayo humwezesha kujisikia na kujua umuhimu wa elimu hiyo.

Alisema ameamua kutoa msaada huo ili kuhakikisha wanafunzi hao wanakuwa mfano bora wa kufaulu masomo yao pasipo pingamizi.

Aidha, alisema kitendo cha yeye kutoa msaada huo ni miongoni mwa utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020/2025.

Kwa upande wao walimu kutoka shule zilizopatiwa msaada huo, waliahidi kuvitumia na kuvitunza ipasavyo vifaa hivyo kama ilivyokusudiwa.

Msaidizi Mwalimu Mkuu wa Shule ya Bwefum, Bahati Bashiru, alisema msaada huo wameupokea na umekuja wakati mwafaka ambao wanafunzi wana uhitaji mkubwa hasa katika kipindi hiki wanapojiandaa na mitihani yao ya taifa.

Naye mwanafunzi Othman Ali wa Shule ya Kombeni Sekondari, alisema msaada wa vifaa hivyo utakuwa chachu ya wao kufanya bidii na kufaulu katika mitihani yao.

"Umetupatia msaada huu kwa moyo wako na sisi tunakuahidi tutatoa matunda mazuri katika shule zetu," alisema.

# Tume yatakiwa mbinu mpya kupambana na UKIMWI

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Dk Omar Dadi Shajak, ameitaka Tume ya UKIMWI Zanzibar kukabiliana vyema na mazingira ya sasa kwa kutumia mbinu na kuibua mawazo mapya ambayo yatazidisha mapambano dhidi ya maambukizi hayo.

Aliyasema hayo jana alipofanya mazungumzo na viongozi pamoja na watendaji wa Tume ya UKIMWI Ofisini kwake Migombeni Mjini Zanzibar, na kusema kuwa jitihada zinazofanyika sasa katika kukabiliana na maambukizi yaende mbali zaidi kwa vile dunia hivi sasa nguvu kubwa imewekeza kwenye kupambana na virusi vya Corona.

Alisema ugonjwa wa corona umeifanya jamii kujisahau kuwa ugonjwa wa UKIMWI bado upo na kwamba Tume hiyo iendelee kuchukua nafasi yake katika kuelimisha jamii na kuhakikisha hakuna maambukizi mapya ya VVU ifikapo mwaka 2025.

"Juhudi zetu zilenge mafanikio na kufikiria njia mbadala za kutatua matatizo yaliyopo, mpango mkakati wa nne ni vyema sasa ukaangalia mawazo mapya yatakayotuvusha hapa tulipo ili tuondokane na maradhi ya UKIMWI," alisema.

Aliwataka watendaji wa tume hiyo pia kuhakikisha lengo la kupunguza na kuondokana na idadi ya maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto linafikiwa, vijana na makundi maalum kupewa elimu na wenye mahitaji kupatiwa dawa na tiba sahihi

Naye Mkurugenzi Mtendaji Tume ya UKIMWI, Dk. Ahmeid Muhamed Khatib, alisema katika kufikia malengo ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Tume ina wajibu wa kutayarisha mkakati maalum na wadau wote wanajukumu la kuufuata mkakati huo.

"Tume ya UKIMWI inaendelea na matayarisho ya mkakati wa nne utaogusa sekta zote kama taasisi za serikali ama binafsi pamoja na jamii kwa vile wadau wote ni wa mapambano na hivyo ni wajibu wa kila anaeguswa kuhakikisha malengo ya nchi na dunia yanafikiwa," alisema.

Alisema mafanikio yaliyopatikana katika kudhibiti maradhi ya UKIMWI yamesababisha kufikia chini ya asilimia moja ya kiwango cha maambukizi na nchi chache zimefikia malengo hayo na kuifanya Zanzibar iwe ni moja kati ya nchi zenye mafanikio.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA ENTEPRISES FINANCE LIMITED (EFL). KWA MAWASILIANO ZAIDI **TUPIGIE:0677 111 333 AU 0758 112 332**

MFAMASIA ANAHITAJIKA

ANAHITAJIKA MFAMASIA MWENYE LESENI YA BODI MADUKANI PHAMACY SINZA DAR ES SALAAM. SIMU NAMBA 0745 181910.


**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika Mahakama ya Mwanzo MJINI TANGA**
**Usimamizi wa Mirathi No. 159/2021**
**Ombi la RASHIDI YUSUFU BAMVUA Kuteuliwa**
**Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu YUSUFU RASHIDI BAMVUA**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo **tarehe 8/10/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe 22/09/2021.**




116485502

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

MARCO MUGIZI AUDAX anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye namba MC 507 CQT wakati akienda kazini.Taarifa za kupotea zimetolewa katika kituo cha Polisi Muleba na kufunguliwa jalada namba KAG/MUL/RB/854980/2020.Atakayeiona atoe taarifa katika kituo chochote cha Polisi.

116485702

## KUPOTELEWA NA HATI MILIKI YA NYUMBA

FAMILIA YA MAREHEMU **WATSON SAKAI MWAKALILA** WANATANGAZA KUPOTELEWA NA HATI MILIKI YA NYUMBA YENYE **BLOCK NO 542** ILIYOPO SOWETO MBEYA. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/465987/2021**.

116485802

**KIBAIGWA AUCTION MART & CO. LTD COURT BROKER**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

TUTAFANYA MNADA TAREHE **29/10/2021 SAA NNE** ASUBUHI WA KUUZA GARI AINA YA **SCANIA KIBINI T 434 DQY, TRAILER SCANIA T 453 AQJ** MALI YA JAMIRI ALLY RASHID, BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MKOPO ALIYOKOPA IMARISHA MAISHA LIMITED, **P.O. BOX4169 DODOMA.** MNADA UTAFANYIKA NYERERE SQUARE, HIVYO TUNAPENDA KUWATANGAZIA WAHITAJI WOTE.

**KWA MAWASILIANAO PIGA NO. 0688729841/0784718272.**

116485902

**KIBAIGWA AUCTION MART & CO. LTD COURT BROKER**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

TUTAFANYA MNADA TAREHE 29/10/2021 SAA NNE ASUBUHI WA KUUZA GARI AINA YA BREVIS T 401 DKR, MALI YA CHRISTOPHER K. ABBAS, BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MKOPO ALIYOKOPA IMARISHA MAISHA LIMITED, P.O. BOX4169 DODOMA. MNADA UTAFANYIKA NYERERE SQUARE, HIVYO TUNAPENDA KUWATANGAZIA WAHITAJI WOTE.

**KWA MAWASILIANAO PIGA NO. 0688729841/0784718272.**

116485902

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ALLY MOHAMED MALIK** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA NOAH YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 729 DUL** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI **KAH/ RB/496/2021**

116486402

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

116460202

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Rais Nicolas Sarkozy afungwa mwaka mmoja

**Paris, UFARANSA**

RAIS mstaafu wa Ufaransa Nicolas Sarkozy, amehukumiwa kifungo cha nyumbani, mwaka mmoja kwa kosa la kufadhili kampeni, kwenye uchaguzi mkuu mwaka 2012, ingawa alishindwa kuupata urais.

Wakili wake Thierry Herzog, amesema mteja wake, ambaye hakuwapo mahakamani hukumu ikitolewa, anaweza kukata rufaa.

Sarkozy ambaye inadaiwa alitumia kiasi cha fedha mara mbili ya kile kinachoruhusiwa kisheria, Euro milioni 22.5, sawa na dola milioni 27.5 milion, kwenye kampeni dhidi ya mpinzani wake, Msoshalisti Francois Hollande.

Sarkozy, alikuwa rais wa Ufaransa kuanzia mwaka 2007 hadi 2012, alikanusha tuhuma hizo, wakati wa kesi hiyo, hapo awali.

Korti ilisema Sarkozy ataruhusiwa kutumikia kifungo cha mwaka mmoja nyumbani na atatakiwa kuvaa kifaa maalumu, ambacho ni bangili ya kielektroniki, ili kumfuatilia.

Wakili wa Sarkozy, Thierry Herzog, alibaini kuwa adhabu hiyo, inalingana na kiwango cha juu cha mteja wake. Alisema alikuwa amezungumza na Sarkozy, ambaye alikuwa amemwomba akate rufaa.

"Hukumu haitatekelezwa" inasubiri rufaa, aliongeza.

Sarkozy alikuwa na mashtaka yanayohusu matumizi ya pesa haramu katika kampeni ya uchaguzi alioshindwa mwaka 2012.

Viongozi wa mashtaka walisema kuwa Sarkozy katika kampeni alitumia kampuni ya uhusiano Bygmalion, kutoa risiti kwa chama chake badala ya kutoa risiti kwa kamati kuu ya kampeni yake, kwa kazi iliyofanywa katika kampeni yake.

Watu wengine 13 pia nao walihusishwa na mashtaka hayo.

Alishindwa kwenye uchaguzi huo na Francois Hollande na kushindwa tena kupata nafasi ya kuwania uchaguzi wa urais.

**AP/BBC**




Thierry Herzog, wakili wa aliyekuwa Rais wa Ufaransa, Nicolas Sarkozy (katikati), akiwasili mahakamani jijini Paris, nchini Ufaransa, kusikiliza kesi ya mteja wake, huku mahakama ikimhukumu Sarkozy, kifungo cha nyumbani mwaka mmoja, jana, kwa kosa la matumizi mabaya ya fedha katika kampeni ya uchaguzi, alioshindwa mwaka 2012. **PICHA; AP**

# Makundi hasimu yaua 100 gerezani

**Guayaquil, ECUADOR**

RAIS wa Ecuador Guillermo Lasso ametangaza hali ya hatari katika magereza yote ya Ecuador, siku moja baada ya mapigano kati ya magenge hasimu, ambayo yalisababisha vifo vya zaidi ya watu 100 katika gereza moja Kusini Magharibi mwa nchi hiyo.

"Nimetangaza hali ya hatari katika magereza yote nchini," alisema Guillermo Lasso, kwenye ukurasa wake wa Twitter, wakati magereza ya Ecuador kwa miezi kadhaa yamekuwa yakikumbwa vurugu za mara kwa mara kati ya makundi ya wahalifu yanayohusishwa na biashara haramu ya dawa za kulevya.

"Huko Gayaquil, nitasimamia kamati ya usalama inayohusika na kuratibu hatua zinazohitajika kudhibiti dharura, kwa kuhakikisha haki za binadamu za kwa watu wote waliohusika zinaheshimishwa," aliongeza.

Makabiliano hayo ni mabaya zaidi, mwaka huu, yalifanyika katika gereza kuu la Guayas, huko Guayaquil, Mji wa bandari na kitovu cha biashara kusini Magharibi mwa nchi.

"Zaidi ya wafungwa 100 waliuawa na 52, walijeruhiwa" wakati wa vurugu, Mamlaka ya Magereza (SNAI) ilitangaza juzi.

Ripoti ya awali, iliyotolewa na Kamanda wa Polisi wa Guayaquil Jenerali Fausto Buenano, ambaye aliongoza operesheni hizo kudhibiti tena majengo ya jela, ilibaini kwamba wafungwa 30 waliouawa katika mapigano, sita kati yao walikatwa vichwa.

**RFI**

## Laschet, Merkel wampongeza Scholz

**Berlin, UJERUMANI**

WAKATI juhudi za kutafuta maelewano ya kuunda serikali nchini Ujerumani zinaendelea na Kansela Angela Merkel na mgombea aliyewania kumrithi kutoka kambi yake ya wahafidhina, Armin Laschet, wamempongeza mgombea wa SPD Olaf Scholz, aliyeshinda uchaguzi huo wa Jumapili.

Msemaji wa Kansela Angela Merkel, ameeleza, kwamba Kansela amempongeza Olaf Scholz kwa mafanikio aliyoyapata kwenye uchaguzi, wakati Chama cha Christian CDU kikisema, Armin Laschet ametoa pongezi zake kwa Scholz.

Laschet alikuwa akikosolewa sana kwa kushindwa kumpongeza mapema mpinzani wake huyo, aliyeshinda uchaguzi, mwishoni mwa wiki.

Matokeo ya uchaguzi yameitumbukiza kambi ya wahafidhina kwenye mgogoro, baadhi ya vigogo wa juu wameonyesha kujiweka kando na Armin Laschet, kiongozi wa CDU kusisitiza muda wote kwamba atajaribu kuunda serikali mpya ya mseto licha ya kushika nafasi ya pili kwenye uchaguzi wa Jumapili.

Kansela Merkel, ambaye anaondoka baada ya miaka 16 madarakani alikuwa kimya kipindi chote, ameuvunja ukimya huo, kupitia taarifa hiyo, iliyotolewa inayoonyesha kwamba alimpongeza Scholz tangu Jumatatu.

Scholz ambaye ni waziri wa fedha katika serikali ya mseto ya Kansela Merkel, anatafuta namna ya kufikia makubaliano na Chama cha Kijani, kilichopata asilimia 14.8 ya kura pamoja na Free Democratic Party (FDP), kilichopata asilimia 11.5 ya kuunda serikali mpya angalau kufikia Desemba na anasema amekabidhiwa mamlaka na wapiga kura kuunda serikali ikiwezekana.

Jana, Naibu Kiongozi wa Chama cha CDU, ambaye ni Waziri wa Afya, Jahn Spahn, akizungumza na kituo cha redio cha taifa cha DeutschlandFunk alisema vyama vya kisiasa vinapaswa kufikia mwafaka kufikia katikati ya mwezi Oktoba.

Chama cha kijani cha wanamazingira walisema kwamba duru yao ya mwanzo ya mazungumzo ya ufafanuzi na Waliberali FDP, ilikwenda vizuri ingawa ulijitokeza mvutano kuhusu ni chama gani kikubwa kati ya SPD na CDU wanachotaka kuingia nacho, kwenye serikali mpya.

**DW**

**Kansela Merkel, ambaye anaondoka baada ya miaka 16 madarakani alikuwa kimya kipindi chote, ameuvunja ukimya huo, kupitia taarifa hiyo, iliyotolewa inayoonyesha...**

# DTB YAWEKA MIKAKATI KUPANDA LIGI KUU BARA

**Na Saada Akida**

WAKATI kinyang'anyiro cha kuwania ubingwa wa Ligi ya Championship, kinatarajiwa kuanza kesho kwenye viwanja mbalimbali hapa nchini, Kocha Mkuu wa DTB FC, Ramadhani Nsanzurwimo amesema kikosi chake kimejiandaa vyema kuhakikisha wanapata matokeo chanya katika mchezo wao wa kwanza wa ligi hiyo.

DTB itafungua dimba la michuano hiyo zamani ikijulikana kama Ligi Daraja la Kwanza kwa kucheza dhidi ya African Lyon kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Nsanzurwimo alisema wachezaji wake wako tayari kuwakabili wapinzani wao na wameahidi kuondoka na ushindi katika mchezo huo wa ufunguzi.

Nsanzurwimo alisema anatambua mechi hiyo itakuwa na ushindani kwa sababu wanakutana na timu yenye uzoefu kwenye ligi hiyo na wataingia uwanjani wakiwawaheshimu wapinzani wao.

Alisema wachezaji wake wameimarika na anaamini mazoezi ya muda mrefu waliyofanya yatawasaidia kufikia malengo.

"Tunawaheshimu sana, African Lyon ni wazoefu kwenye hii ligi, wako muda mrefu na wachezaji wake wamezoeana tofauti na timu yangu imetoka daraja la pili na kufanya usajili mwingine," alisema Nsanzurwimo.

Kocha huyo aliongeza ana matumaini na usajili waliofanya kwa sababu waliangalia wachezaji wenye uzoefu na wenye uwezo wa kuhimili ushindani.

DTB FC inaundwa na 'mastaa' ambao waliwahi kuzitumika klabu mbalimbali za Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwamo Simba, Yanga, Mbeya City na Singida United.

Baadhi ya nyota wanaounda kikosi hicho ni pamoja na Mrundi Amisi Tambwe, Juma Abdul, Yusuph Mlipili, Owen Chaima, Shafiq Batambuzi na Tafadzwa Kutinyu ambaye kwa sasa ni majeruhi.



Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Suma JKT, Kanali Respicius Kaiza (Watatu kutoka kulia) na Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Sanaa kutoka Wizara ya Sanaa, Utamaduni na Michezo, Leah Kihimbi (anayemfuata), wakiwa na waandaaji pamoja na washiriki wa shindano la Miss na Mr Kiziwi kutoka Tanzania. **PICHA: ROMANA MALLYA**

# Miss, Mr Kiziwi kupatikana leo

**Na Romana Mallya**

SHINDANO la kumsaka Miss na Mr Kiziwi linatarajia kufanyika leo kwenye Kituo cha mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere jijini Dar es Salaam kwa kushirikisha warembo kutoka nchi 12 hapa barani Afrika.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa SumaJKT, Kanali Respicius Kaiza alisema taasisi hiyo imedhamini shindano hilo kwa sababu wanaamini mshindi atakayepatikana atakuwa Mtanzania atapata nafasi ya kuitangaza nchi kimataifa.

Kanali Kaiza alikipongeza Kikundi cha Sanaa na Utamaduni cha Viziwi Tanzania (KISUVITA) kwa kuandaa shindano hilo.

"KISUVITA iliomba udhamini kwetu na uongozi uliona ni jambo jema kwa sababu tunaamini akishinda Mtanzania atapata nafasi ya kuitangaza nchi kimataifa na maliasili tulizonazo ukiwamo mlima Kilimanjaro," alisema Kaiza.

Mkurugenzi wa KISUVITA, Habibu Mrope alilishukuru jeshi hilo kwa udhamini waliotoa na kutambua thamani ya kundi hilo huku akiongeza Tanzania ilianza kushiriki mashindano hayo ya kimataifa tangu mwaka 2019.

Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Sanaa kutoka Wizara ya Sanaa Utamaduni na Michezo, Leah Kihimbi alisema nchi 31 zilialikwa lakini zilizothibitisha kushiriki ni 12 ambazo ni Kenya, Burundi, Botswana, Sierra Leone, Senegal, Sudan Kusini, Msumbiji, Uganda, Rwanda, Zambia, Zimbabwe na wenyeji Tanzania.

## Namungo hofu ikiifuata Kagera

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Namungo FC, Hemed Morocco, amesema mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Kagera Sugar utakaochezwa keshokutwa unatarajiwa kuwa mgumu kwa sababu ya kiwango bora kilichoonyeshwa na wapinzani wao hapo juzi.

Licha ya kulala bao 1-0, Kagera Sugar ilionyesha kiwango cha juu ilipowakaribisha Yanga katika mchezo wa ufunguzi wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliochezwa juzi kwenye Uwanja wa Kaitaba Mjini Bukoba.

Morocco aliliambia gazeti hili Kagera Sugar imeimarika na wachezaji wake wanatakiwa kuongeza umakini ili kuhakikisha wanapata ushindi.

"Kwa namna nilivyowaangalia jana (juzi), ninaona mechi yetu itakuwa ngumu na yenye ushindani mkubwa," alisema Morocco.

Kocha huyo alisema ameshafahamu mazuri na madhaifu ya Kagera Sugar, hivyo atawapanga vyema wachezaji wake na hatimaye kuendelea kupata ushindi kwenye ligi hiyo.

"Hatuna majeruhi, tunatambua mechi itakuwa ngumu, Kagera Sugar wameimarika sana na sisi hatutaingia kichwa kichwa hata kama tunacheza nyumbani, ubora wetu na wao utaufanya mchezo kuwa mzuri na kuvutia," alisema Morocco.

## Bridge Star yaota makubwa Z'bar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Bridge Star inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja imesema imejipanga vizuri kuhakikisha inafanya vyema kwa ajili ya kutimiza malengo yake ya kupanda daraja, imefahamika.

Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja itakayoshirikisha timu 16 inatarajiwa kufanyika kuanzia Oktoba mwishoni.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa Bridge Star, Iddi Meya, alisema wanaamini watafanya vizuri kutokana na usajili wa wachezaji wenye uzoefu waliofanya tangu dirisha la usajili lilipofunguliwa.

Meya alisema usajili umezingatia wachezaji ambao watahimili mikikimikiki na ushindani wa ligi ambayo inatarajiwa kuwa ngumu kutokana na kila timu kuhitaji kupanda daraja.

"Tunatarajia kusajili wachezaji sita wapya ambao wataungana na nyota 22 wa zamani walioipandisha daraja timu hiyo iliyotokea ligi ya mkoa wa Kusini," Meya alisema.

Baadhi ya timu nyingine zitakazoshiriki Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja ni pamoja na New Power, Paje Star, Wembe FC, African Coast, Umoja wa Mbuzini na Kundemba FC.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**LACAZETTE HUYO SEVILLA**
ARSENAL itamtoa mshambuliaji wa Ufaransa, Alexandre Lacazette mwenye umri wa miaka 30, kwa Sevilla kama sehemu ya makubaliano ya kumsajili mshambuliaji wa Morocco wa miaka 25, Youssef En-Nesyri. **(La Razon)**

**PHILLIPS KITAELEWEKA**
LEEDS United wameanza mazungumzo ya mkataba na kiungo wa kati wa England, Kalvin Phillips kwa nia ya kutompoteza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 kwa wapinzani wao wa Ligi Kuu England, Manchester United. (Star)

**SPURS YAINGIA SOKONI**
KLABU ya Tottenham Hotspur wanajipanga kumsajili golikipa wa West Brom na England, Sam Johnstone mwenye umri wa miaka 28**. (Football Insider)**

**WINKS NJIA MOJA**
TOTTENHAM Hotspur wamesema wako tayari kumwachia kiungo wa kati wa England, Harry Winks mwenye umri wa miaka 25, kuondoka klabuni hapo wakati wa dirisha la Januari. **(Caughtoffside)**

**RICE: SIONDOKI WEST**
KIUNGO wa kati wa England, Declan Rice amesema anaridhika kuwa West Ham na anaweza kufikia malengo yake. Rice mwenye umri wa miaka 22 amekuwa akihusishwa na tetesi za kujiunga na Chelsea na Manchester **United. (Sky Sports)**

**WIRTZ ANUKIA CITY**
MANCHESTER City wanamnyatia kiungo wa kati wa Bayern Leverkusen mwenye umri wa miaka 18 raia wa Ujerumani, Florian Wirtz. **(Bild via Sport Witness)**

**CHELSEA YAMTAKA TORRES**
CHELSEA wanafikiria kumsajili nyota wa Villarreal, Pau Torres mwenye umri wa miaka 24. Manchester United pia wanamtaka raia huyo wa Hispania. **(90min)**

**ONANA AKARIBIA INTER**
KLABU ya Inter Milan haitaki kumsajili golikipa wa Arsenal na Ujerumani, Bernd Leno mwenye umri wa miaka 29. Klabu hiyo ya Serie A badala yake inamsaka mchezaji wa kimataifa wa Cameroon, Andre Onana mwenye umri wa miaka 25 kutoka Ajax. **(Fabrizio Romano via Twitter)**

**KOUNDE NA SEVILLA**
JULES Kounde amesema ataizingatia Sevilla baada ya dau la Chelsea kushindwa kumsaini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 kipindi cha majira ya joto. **(Star)**

**VLAHOVIC AGOMBEWA**
RAIS wa Fiorentina, Rocco Commisso, amesema klabu hiyo inajizatiti kumshawishi Dusan Vlahovic ambaye anawindwa Arsenal na Chelsea kusaini mkataba mpya. mshambuliaji huyo wa Serbia mwenye umri wa miaka miaka 21 alifunga mabao 21 ya Serie A msimu uliopita. **(Express)**

**VILLAR ATAKIWA EVERTON**
EVERTON wanamfuatilia kiungo wa kati wa AS Roma, Gonzalo Villar ambaye ana umri wa miaka 23, baada ya kubaini mchezaji huyo hayupo katika mipango ya Kocha, Jose Mourinho. **(Fichajes)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO AZIDI KUNG'ARA UEFA

Ni baada ya mshambuliaji huyo kuweka rekodi mpya katika Ligi ya Mabingwa...

**MANCHESTER, England**

CRISTIANO Ronaldo ameweka rekodi ya mchezaji aliyecheza mechi nyingi zaidi kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati Manchester United ikiibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Villarreal juzi Jumatano.

Raia huyo wa Ureno aliifikia rekodi ya golikipa wa zamani wa Real Madrid na Porto, Iker Casillas kwa kufikisha mechi 177 kwenye mashindano hayo ya Ulaya wakati alipocheza dhidi ya Young Boys wiki iliyopita.

Lakini sasa Ronaldo ameweka rekodi yake ya kuwa mchezaji aliyecheza mechi nyingi zaidi kwenye michuano hiyo baada ya kushuka dimbani pale kwenye Uwanja wa Old Trafford, juzi.

Ronaldo ameanza katika mechi zote tatu za Ligi Kuu England kwa United tangu aliporudi kwa mara ya pili katika klabu hiyo, akifunga jumla ya mabao matano pamoja na kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Akizungumza baada ya mchezo wa juzi ambapo Ronaldo akifunga bao la ushindi katika dakika za majeruhi, Kocha, Ole Gunnar Solskjaer alimsifia nyota huyo kwa kuwa na uwezo mkubwa wa kufunga.

Alisema: "Bila shaka ukiwa na Cristiano una uhakika wa kupata bao wakati wowote, ana rekodi hiyo ya kufunga mabao.

"Haikuwa kazi rahisi kucheza dhidi ya Villarreal, lakini Cristiano ndio aliweka rekodi."

MECHI KALI
HOME AWAY
BIASHARA UNITED
1.62 | 3.28 | 5.79
RUVU SHOOTING
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 537
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa
halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KOEMAN AKUBALI HANA MAISHA BARCELONA



**LISBON, Ureno**

RONALD Koeman anaamini licha wachezaji wa Barcelona kumuunga mkono, lakini haoni majaliwa yake ya baadaye kwenye timu hiyo baada ya kukumbana na kichapo cha mabao 3-0 kutoka kwa Benfica kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyochezwa juzi.

Barca walifungwa idadi kama hiyo ya mabao kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya makundi dhidi ya Bayern Munich na wakanyanyaswa tena juzi Jumatano hapa jijini Lisbon.

Inamaana Barca wamepoteza mechi zao mbili za kwanza za Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya kwanza na sasa wanashika mkia kwenye Kundi E.

Juu ya hilo, Barca wamepoteza mechi mfululizo hatua ya makundi kwa mara ya kwanza tangu msimu wa 2000/01.

Barca wametoka kumpoteza nyota wao muhimu, Lionel Messi aliyetimkia PSG baada ya kubanwa na sheria za mishahara ya LaLiga.

"Sijazungumzia hali jinsi ilivyo kwa timu," alisema Koeman akiwaambia waandishi wa habari baada ya kupoteza kwa Benfica.

"Kila mmoja anajua matatizo ya sasa ya Barca. Huwezi kusema lolote kwenye timu ambayo sio ile ya miaka michache iliyopita. Kwangu mimi hili lipo wazi kama maji.

"Siwezi kusema kuhusu majaliwa yangu. Nahisi napewa sapoti kubwa sana na wachezaji pamoja na hali jinsi ilivyo, lakini sijui nini klabu inafikiria.

"Majaliwa yangu hayapo mikononi mwangu, na ndio maana sitaki kujibu swali lolote kuhusu majaliwa yangu. Tutaona nini kitakachotokea. Naikubali dunia ambayo sisi makocha tunaishi."

# Tuchel: Chelsea walichoka, walikosa uhuru



**TURIN, Italia**

CHELSEA walionekana wako taratibu, wamechoka na hawakuwa na uhuru wakati walipofungwa na Juventus Jumatano, kwa mujibu wa Kocha Thomas Tuchel.

Licha ya kumiliki mpira kwa asilimia 70, wabingwa hao watetezi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya walichapwa 1-0 na Juventus, bao lililofungwa na Federico Chiesa katika sekunde ya 10 ndani ya kipindi cha pili pale kwenye dimba la Allianz.

Lilikuwa bao la mapema zaidi la kipindi cha kipindi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na kumfanya Chiesa kuwa Mtaliano wa kwanza kufunga katika mechi nne mfululizo alizoanza kwenye michuano hiyo kwa Juve tangu gwiji Alessandro Del Piero mwaka 1997.

Blues hao walipiga shuti moja tu lililolenga goli ambalo lilipigwa na Romelu Lukaku na kukifanya kikosi cha Kocha Massimiliano Allegri kuwa na nafuu kwenye Kundi H.

"Bila shaka, ni vigumu kwa hali kama hili kuruhusu bao katika sekunde za kwanza za kipindi cha pili.

"Wakati ukijua nini kinachokuja na unakuwa na mfumo mzuri wa ulinzi kwa hakika ilikuwa ngumu zaidi kujilinda. Tulisukumwa kwa kila kitu," alisemaTuchel akiiambia BT Sport.

"Nafikiri hatukuwa na kasi ya kutosha. Tulikuwa na umiliki mzuri katika dakika 12 hadi 15 na tungeweza kuwadhuru zaidi, tulitakiwa kuwa na kasi ya kutosha kuweza kujipatia matokeo."

,737,060

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. 02.10.21 | 17:00 | Derby vs Swansea | 2.52 | 3.22 | 2.72 |
| 2. 02.10.21 | 17:00 | Peterborough vs Bristol City | 2.57 | 3.21 | 2.67 |
| 3. 02.10.21 | 17:00 | Luton Town vs Huddersfield | 2.39 | 3.25 | 2.86 |
| 4. 02.10.21 | 17:00 | Hull City vs Middlesbrough | 2.86 | 3.25 | 2.39 |
| 5. 02.10.21 | 17:00 | Blackpool vs Blackburn | 2.86 | 3.16 | 2.45 |
| 6. 02.10.21 | 17:00 | Barnsley vs Millwall | 2.27 | 3.20 | 3.11 |
| 7. 02.10.21 | 18:00 | Montpellier vs Strasbourg | 2.40 | 3.47 | 2.78 |
| 8. 02.10.21 | 19:30 | Brighton vs Arsenal | 2.85 | 3.15 | 2.58 |
| 9. 02.10.21 | 22:00 | Atletico Madrid vs Barcelona | 2.14 | 3.32 | 3.47 |
| 10. 03.10.21 | 16:00 | Tottenham vs Aston Villa | 2.14 | 3.46 | 3.36 |
| 11. 03.10.21 | 16:00 | Crystal Palace vs Leicester | 3.21 | 3.46 | 2.20 |
| 12. 03.10.21 | 18:00 | Lille vs Marseille | 2.45 | 3.29 | 2.84 |
| 13. 03.10.21 | 18:30 | Liverpool vs Manchester City | 2.75 | 3.39 | 2.52 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 01 - OKTOBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 4355 | Biashara United vs Ruvu Shooting | 1.62 | 3.28 | 5.79 |
| 16:30 | 1019 | Al-Sailiya SC vs Al Khoor | 2.08 | 3.43 | 3.10 |
| 17:30 | 1356 | Barracas Central vs All Boys | 2.12 | 2.96 | 3.49 |
| 18:30 | 1343 | Ayacucho vs Carlos Mannucci | 2.51 | 3.00 | 2.75 |
| 19:00 | 4120 | Zaglebie Lubin vs Jagiellonia | 2.16 | 3.24 | 3.10 |
| 19:00 | 5959 | HNK Sibenik vs HNK Gorica | 2.61 | 3.28 | 2.46 |
| 19:15 | 4648 | Al Arabi Doha SC vs Al Sadd SC | 6.76 | 5.22 | 1.32 |
| 19:30 | 2317 | Werder Bremen vs Heidenheim | 1.96 | 3.54 | 3.54 |
| 20:00 | 1158 | Elfsborg vs IFK Goteborg | 1.66 | 3.68 | 4.55 |
| 20:00 | 1241 | Apollon Limassol vs AEK Larnaca | 1.96 | 3.21 | 4.05 |
| 20:00 | 1423 | Odense vs Vejle BK | 1.60 | 4.05 | 4.94 |
| 20:00 | 4841 | Antalyaspor vs Adana Demirspor | 2.45 | 3.29 | 2.75 |
| 20:00 | 5459 | Fatih Karagumruk vs Basaksehir | 2.42 | 3.32 | 2.77 |
| 21:00 | 1372 | FC Oss vs De Graafschap | 4.50 | 4.11 | 1.61 |
| 21:00 | 1711 | Maritimo vs Moreirense | 2.45 | 3.05 | 2.95 |
| 21:00 | 1812 | Maastricht vs ADO Den Haag | 3.76 | 3.86 | 1.79 |
| 21:00 | 2224 | Helmond Sport vs Jong Ajax | 2.83 | 3.71 | 2.16 |
| 21:00 | 2249 | Jong PSV vs VVV Venlo | 2.32 | 3.41 | 2.78 |
| 21:00 | 2422 | Roda Kerkrade vs FC Eindhoven | 1.63 | 4.01 | 4.49 |
| 21:00 | 2710 | FC Volendam vs Almere City | 1.87 | 3.71 | 3.57 |
| 21:00 | 3158 | Sport Boys Association vs Alianza Atletico | 2.13 | 3.11 | 3.30 |
| 21:00 | 3455 | Jong AZ Alkmaar vs Dordrecht | 1.66 | 4.02 | 4.31 |
| 21:00 | 3600 | Jong Utrecht vs Emmen | 4.00 | 3.85 | 1.74 |
| 21:00 | 3838 | Chindia Targoviste vs Steaua Bucuresti | 4.43 | 3.25 | 1.83 |
| 21:00 | 4565 | Groningen vs Twente | 2.42 | 3.29 | 2.80 |
| 21:00 | 4583 | Den Bosch vs Telstar | 2.49 | 3.66 | 2.44 |
| 21:00 | 4817 | NAC Breda vs SBV Excelsior | 2.25 | 3.53 | 2.79 |
| 21:00 | 5210 | Budapest Honved vs Kisvarda FC | 2.34 | 3.29 | 2.75 |
| 21:00 | 5282 | Deportivo Muniz vs CA Lugano | 2.51 | 2.80 | 2.94 |
| 21:30 | 1087 | Lecce vs Monza | 2.13 | 3.16 | 3.46 |
| 21:30 | 2138 | Bray Wanderers vs Cork City | 2.01 | 3.25 | 3.45 |
| 21:30 | 2653 | FC Vaduz vs FC Thun | 2.01 | 3.63 | 3.10 |
| 21:30 | 2937 | GKS Piast Gliwice vs Wisla Krakow | 2.04 | 3.38 | 3.24 |
| 21:30 | 3834 | FC Koln vs Greuther Furth | 1.48 | 4.66 | 5.75 |
| 21:30 | 5224 | FC Schaffhausen vs Neuchatel Xamax | 2.02 | 3.73 | 3.00 |
| 21:45 | 1233 | Edinburgh City vs Cowdenbeath | 1.74 | 3.83 | 3.88 |
| 21:45 | 1328 | Drogheda Utd vs St Patricks | 3.83 | 3.25 | 1.90 |
| 21:45 | 2660 | Stoke City vs West Bromwich | 3.00 | 3.20 | 2.33 |
| 21:45 | 3335 | Mechelen vs Standard Liege | 2.27 | 3.60 | 2.81 |
| 21:45 | 4708 | Linfield Belfast vs Cliftonville Belfast | 1.61 | 4.17 | 4.27 |
| 21:45 | 5031 | Cagliari vs Venezia | 1.71 | 3.86 | 4.71 |
| 22:00 | 3051 | Athletic Bilbao vs Alaves | 1.56 | 3.86 | 6.41 |
| 22:00 | 3558 | Lens vs Reims | 1.84 | 3.48 | 4.27 |
| 22:00 | 3747 | Shamrock Rovers vs Derry City | 1.46 | 3.96 | 6.38 |
| 22:00 | 4306 | Ponferradina vs Valladolid | 2.91 | 3.06 | 2.47 |
| 22:00 | 4786 | Finn Harps vs Dundalk FC | 3.00 | 3.29 | 2.19 |
| 22:00 | 4825 | Deportivo Maldonado vs CA Rentistas | 2.67 | 3.25 | 2.42 |
| 23:10 | 5650 | Villa Dalmine vs CA Guemes | 2.99 | 2.61 | 2.65 |
| 23:15 | 5865 | Famalicao vs Vitoria Guimaraes | 2.70 | 3.19 | 2.55 |
| 23:30 | 5915 | Club Cienciano vs Sporting Cristal | 5.44 | 3.98 | 1.52 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# NUNO: WACHEZAJI WANA IMANI NA MIMI



**LONDON, England**

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Nuno Espirito Santo, amesisitiza anaungwa mkono na wachezaji licha ya timu hiyo kuwa na matokeo mabaya katika mechi za hivi karibuni.

Spurs ilikuwa na mwanzo mzuri chini ya kocha huyo mpya, wakishinda mechi nne kati ya tano kwenye mashindano yote, huku wakiruhusu bao moja tu.

Kiwango cha hivi karibuni kimekuwa kibaya, wakifungwa 3-0 kwenye Ligi Kuu na Crystal Palace pamoja na Chelsea, wakitoka sare ya 2-2 na Rennes na Wolves kwenye Ligi ya Europa Conference na Kombe la EFL.

Wiki iliyopita, Tottenham wakafungwa mabao 3-1 na majirani zao wa Kaskazini mwa Jiji la London, Arsenal, matokeo ambayo yalianza kutoa ishara mbaya kwa majaliwa ya kocha huyo.

Hata hivyo, Nuno, kocha wa zamani wa Wolves amesema wachezaji wanaamini katika mbinu zake na shutuma kutoka sehemu nyingine hazimsumbui.

Akizungumza kabla ya mchezo wa jana Alhamisi dhidi ya Mura, alisema: "Ndio, kwa uhakika wananiamini sana.

"Hakuna shaka kuhusu hilo kwa sababu tunafanya kazi kwa pamoja kila siku, tunajiandaa pamoja na wachezaji wote wana imani kubwa na mimi hasa kwa mbinu zangu."



# Xhaka kukaa nje ya dimba miezi mitatu

**LONDON, England**

KIUNGO wa Kati wa Arsenal, Granit Xhaka, anatarajiwa kuwa nje ya uwanja kwa miezi mitatu baada ya kuumia goti katika dabi ya London walioibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Tottenham Hotspur.

Xhaka aligongwa kwa bahati mbaya na Lucas Moura baada ya mchezaji huyo kuchezewa madhambi na Thomas Partey na kudondoka chini katika harakati za Tottenham kujitafutia bao la kufuta machozi.

Mchezaji huyo alitolewa nje na nafasi yake kuchukuliwa na Albert Sambi Lokonga na taarifa zilizothibitishwa ni kuwa mchezaji huyo atakosa mwaka wote wa 2021.

"Kwa mujibu wa uchunguzi zaidi uliofanywa katika jeraha la goti la kulia baada ya mechi dhidi ya Tottenham, vipimo vimethibitisha Granit Xhaka amepata jeraha baya katika goti lake," ilisomeka taarifa ya Arsenal.

"Wataalamu walifanya kikao London siku ya Jumanne jioni na kugundua Xhaka hahitaji upasuaji.

"Programu ya kurejea na kupona itaanza mara moja na tunatarajia atarejea baada ya miezi mitatu.

"Kila mtu ndani ya klabu anamsapoti na kufanya kazi kwa bidii na Xhaka kuweza kumrejesha uwanjani haraka iwezekanavyo."

# Michezo

Ijumaa Oktoba 1, 2021

Nipashe


Ronaldo azidi kung'ara UEFA

UKURASA 21





Mshambuliaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), Oppa Clement (kulia), akipambana kuwania mpira dhidi ya mchezaji wa Zimbabwe katika mechi ya mashindano ya COSAFA iliyochezwa jijini Port Elizabeth, Afrika Kusini juzi. Twiga Stars ilishinda mabao 3-0. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA, DODOMA JIJI MAJARIBUNI

## Matola atamba kikosi kiko tayari kurejesha furaha na...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WAKIWA na kumbukumbu ya kulazimishwa sare ya bila kufungana katika mchezo uliopita, mabingwa watetezi, Simba wanatarajia kukutana na Dodoma Jiji FC katika mechi ya raundi ya pili ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

Simba itaingia uwanjani ikiwa na kazi moja ya kuponya vidonda kwa wanachama na mashabiki wake baada ya kufungwa pia bao 1-0 kwenye Ngao ya Jamii iliyochezwa Septemba 25, mwaka huu na matokeo kama hayo katika Tamasha la Simba Day ambalo waliwakaribisha TP Mazembe ya DRC.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Simba, Suleiman Matola, alisema wamerekebisha makosa yaliyojitokeza katika mechi iliyopita dhidi ya Biashara United na sasa wamejiandaa kuondoka na pointi zote tatu muhimu katika mchezo wa leo.

Matola alisema wamejiandaa vyema kuelekea mchezo huo na wanafahamu Ligi Kuu Tanzania Bara ni ngumu na wakati wote watapambana kusaka ushindi.

"Najua mashabiki wanaumia, kiukweli tumejiandaa vizuri, ligi ni ngumu, na sisi tunaumia, tutahakikisha tunawarejeshea furaha yao ambayo walikuwa nayo katika kipindi kilichopita," alisema Matola.

Kiungo huyo wa zamani wa mabingwa hao aliwaomba mashabiki na wanachama kujitokeza kuwashangilia na wanachoahidi ni kuwapa furaha katika mechi hiyo.

Shomari Kapombe, beki wa Simba alisema benchi la ufundi limeyafanyia kazi mapungufu yote na kila mchezaji yuko tayari kuelekea mchezo huo.

"Kikubwa mazoezi ya mwisho yameenda vizuri na programu zote zimemalizika, matumaini yangu makubwa kila mchezaji amejiandaa vizuri kiakili kwa ajili ya mchezo wa kesho (leo), ambao tunahitaji pointi tatu," Kapombe alisema kwa kifupi.

Naye Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, amewatoa hofu wanachama na mashabiki wa timu hiyo kwa kusema kikosi kiko vizuri na matokeo yaliyopita ni ya kawaida na hasa kwa timu ambayo inatoka kwenye maandalizi ya mwanzo ya msimu.

Rweyemamu alisema wataingia uwanjani leo kwa kuwaheshimu wapinzani wao Dodoma Jiji, lakini ana imani wataibuka na ushindi.

"Ligi ni ngumu na nilazima umuheshimu mpinzani wako, tumekuja kusaka pointi tatu, yale yaliyotokea nyuma tumeyaacha kwa sababu tulipata pointi moja, hatukupoteza kabisa, ndiyo kwanza timu imetoka kwenye maandalizi ya mwanzo ya msimu, bado muunganiko wa wachezaji haujaanza kufanya kazi. Ninachosema ni kwamba hii ni ligi, hivyo mwenye pointi nyingi mwishoni ndiyo bingw, ile ilikuwa ni mechi ya kwanza," Rweyemamu alisema.

Ofisa Habari wa Dodoma Jiji, Moses Mpinga, alisema lengo lao ni kukusanya pointi sita za michezo miwili ya kwanza ambayo watacheza kwenye uwanja wa nyumbani na tayari wameshapata pointi tatu mkononi.

"Tayari alama tatu tunazo mkononi, nyingine sasa zitapatikana kwenye mechi dhidi ya Simba. Wamekuja wenyewe machinjioni, tunakula kichwa," alitamba Mpunga.

Mechi nyingine ya ligi hiyo inayotoa wawakilishi katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa leo ni kati ya Biashara United dhidi ya Ruvu Shooting kutoka Mlandizi mkoani Pwani.

## Yanga yafunguka ilipowazidi Kagera

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar, Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze ameweka wazi timu yao haikuonyesha kiwango kizuri katika mchezo huo uliochezwa kwenye Uwanja wa Kaitaba Mjini Bukoba juzi.

Kaze aliliambia gazeti hili sababu kubwa ya kutoonyesha kiwango kizuri ni kutokana na kutumia nguvu nyingi kwenye mchezo uliotangulia wa kuwania Ngao ya Jamii ambao walikutana na watani zao, Simba.

Kocha huyo alisema hali hiyo waliitarajia lakini wanawapongeza wachezaji wao kwa kutumia uzoefu na hatimaye kuondoka na pointi zao tatu muhimu.

"Hatukuridhishwa na kiwango cha leo (juzi), lakini tunajivunia kupata pointi tatu. Tulicheza mchezo mgumu wa Ngao ya Jamii dhidi ya Simba, tulitumia nguvu nyingi kwa hiyo tulijua leo (juzi), hatuwezi kuwa na nguvu kama zile tena. Wachezaji wetu bado hawajarudisha nguvu kwa sababu mechi hiyo haikuchezwa muda mrefu, lakini kitu kizuri tumeshinda," alisema Kaze.

Aliongeza kama wangekuwa makini katika kipindi cha kwanza wangepata mabao matatu au manne, lakini walishindwa kuzitumia nafasi walizozitengeneza.

"Kama unaongoza bao moja, halafu unashindwa kutumia nafasi, unampa nguvu mpinzani wako. Na ndivyo ilivyotokea. Ukiondoa kufunga mabao, lakini umeona sasa wachezaji wanacheza kwa kupishana, wanafika hadi mbele ya goli. Kama wanafanya hivyo, basi kuna mambo kidogo ya kurekebisha ili timu iweze kutumia nafasi inazozipata," Kaze alisema. Naye Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Francis Baraza alisema ameridhishwa na vijana wake, lakini akikiri amefungwa na timu bora.

"Tumefungwa na timu bora, nilisema hivyo tangu awali, lakini nimeridhika na vijana wangu. Kuna makosa madogo tumeyafanya kama yaliozaa bao, tutarudi mazoezini kuyafanyia kazi. Kuna wachezaji wetu wa kigeni ambao bado hawajapata vibali naamini watatusaidia kuelekea mchezo wetu wa pili dhidi ya Namungo," alisema Baraza.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >